


KUSHIRIKIANA KATIKA JUMUIA YA KRISTO


Kuchunguza, Kitambulisho, Misheni, Ujumbe, na Imani

Jumuia ya Kristo

Kwa wale wanaotafuta nyumba ya kiroho,

Jumuia ya Kristo ni jamii ya imani
inayokaribisha,
Yenye upendo, na jamii ya imani ya
kiulimwengu,
Ambayo inathamini thamani ya kila
Mtu kama mtoto wa Mungu na
Hutoa nafasi salama kwako
Kuchunguza na kuimarisha
Uhusiano wako na
Yesu Kristo na kila mmoja.

Katika Jumuia ya Kristo,
Utapokea upendo na
Msaada wakati utagundua
Kusudi jipya la maisha yako
Kupitia huduma ya huruma,
Kama ya Kristo inayomaliza
Mateso na kukuza
Haki na Amani.



YALIYOMO

© 2018
Jumba la uchapishaji la Herald
Independence, Missouri
Haki zote zimehitafadhiwa

@ 2009, 2012 jumba la uchapishaji la Herald
Toleo la kwanza 2009. Toleo la pili 2012. Toleo la tatu 2012 Ilichapishwa Marekani.

ISBN: 978-0-8309-1715-0

Msalaba uliyo juu: Msalaba huu unaninginia katika hekalu ilioko Independence, Missouri. Umetengenezwa kwa kutumia karibu aina 100 za mbao za dunia nzima, Kuwakilisha Zaidi ya mataifa 50 ambayo kanisa limeimarika ndani ya mataifa hayo. Matawi ya mzeituni yaliyo katikati ya msalaba huu yana umbo la njiwa anayeshuka, Kuashiria Amani.
Msanii: David Martin

Kitabu cha kushirikiana katika Jumuiya ya Kristo imeundwa na Jeff Piedmonte.

Utangulizi 6
Mwaliko 8
Tunashirikiana 9
Maono ya uumbaji 9
Jina 11
Siku za usoni 13
Amani ya Yesu Kristo 13
Hadithi takatifu 16
Misheni 20
Kanuni za kudumu na mambo ya msingi ya imani 26
Kanuni za kudumu 27
Mambo ya msingi ya imani 33
Uwakili wa maisha yote 39
Sakramenti 44
Hekalu kama ishara ya kutoa uzima 51
Tunamtangaza Yesu Kristo 58
Maandiko katika jumuia ya Kristo 63
Sisi ni kitu kimoja, Sisi ni wengi 68
Mitazamo kuhusu Historia ya Kanisa 76
Muhtasari 82



UTANGULIZI

Waraka huu wa Tunashirikiana Kitambulisho, Misheni, Ujumbe, na Imani uliwasilishwa kwa kanisa mnamo mwaka wa 2009 kwa kauli ifuatayo:

> Waraka huu umetokana na juhudi za pamoja za wawakilishi wa kanisa la ulimwengu mzima na viongozi wa kanisa. Baraza la uongozi la kanisa la ulimwengu mzima lililopanuliwa, viongozi mbalimbali wa kanisa la ulimwengu mzima, makundi, na watu wengi binafsi wamechangia mambo yaliyo ndani ya waraka huu.
>
> Tunatarajia kwamba waraka huu utafanya kazi muhimu ya kuliongoza kanisa katika



miaka ijayo. Unatoa msingi wa masomo, mahubiri, mitindo ya huduma, vifaa, na shughuli za makundi madogomadogo na matukio ya ibada yanayowanenea watu tunaohudumia. Waraka huu unatoa vifaa muhimu vya kutumia kuelezea kwa njia ya pekee maono na misheni ya Jumuia ya Kristo kote ulimwenguni.

Ukiwa katika hali ya maombi, tafadhali tafakari juu ya taarifa hii, Chukua muda wa kuyashirikisha Zaidi mambo hayo katika maisha yako kama mwanafunzi na pia kama kiongozi. Halafu kwa kutumia vipawa na uzoefu wako, buni njia za kuwasaidia watafutaji, wanafunzi, na kusanyiko kupata maana na tumaini kupitia kwa maono, misheni, ujumbe, na mambo ya imani yaliyowasilishwa ndani ya waraka huu.

Waraka huu si mpango mpya unaohitaji kuzinduliwa na sherehe kuu! Bali ni chumvi na kichocheo cha kusitawisha misheni na ushuhuda wetu tunapoendelea na safari yetu katika siku za usoni.

Toleo la nne la Kushirikiana katika Jumuiya ya Kristo: kuchunguza kitambulisho, misheni, ujumbe, na Imani ni pamoja na mipango mitano ya kubadilisha maisha, kubadilisha kanisa, na mabadiliko ya ulimwengu. Itumie kwa kumbukumbu na kusoma, na kutafakari unapoendelea kuwa katika uanafunzi na kuishi misheni ya Kristo.



MWALIKO

Katika waraka huu kuna mkusanyiko wa maandishi yanayoeleza na kufafanua sisi ni kina nani kama kanisa linalokua katika kazi yetu maalum ya kumtangaza Yesu Kristo na kukuza jumuia za furaha, tumaini, upendo na amani. Unaposoma na kuchunguza hali mbalimbali zinazoeleza "Sisi ni nani" na "Sisi tunanuia kua vipi" soma ukiwa na matarajio yaliyo wazi na kwa hali ya maombi.

Unapo jifunza, shirikiana na wengine katika mazingira ya kutafuta utambuzi mpya unaokua wa roho wa Mungu anayefanya kazi ndani ya maisha yako na vile vile ndani ya maisha ya wanafunzi wengine waaminifu. Soma maandiko yaliyopendekezwa, jibu maswali ya kutafakari, na ufikirie vile maandiko hayo yanavyoarifu maisha yako na uanafunzi wako. Zingatia kwa makini namna ya kuzidisha ubora katika maisha yako na huduma yako kwa kuitikia ushawishi wa Mungu nakufuata mfano wa maisha na huduma ya Yesu.

Picha haki miliki © Brian Jackson | Adobe Stock Foto



TUNASHIRIKIANA....

Neno "Tunashirikiana" limetumiwa katika vichwa vya waraka mzima. Neno hili lina maana mbili muhimu: o "Tunashirikiana" limetumiwa katika vichwa vya waraka mzima. Neno hili lina maana mbili muhimu:

1. Kile tunachoshirikiana pamoja kama washirika na washiriki katika Jumuia ya Kristo huunda kitambulisho, misheni, ujumbe na mambo ya msingi ya Imani kama jumuia ya imani kote ulimwenguni.
2. Ni muhimu kusema kwamba, neno "Tunashirikiana" linasisitiza wito wetu na kujitolea kwetu kushiriki na ulimwengu wote ushuhuda, huduma, sakramenti, vifaa, na ujumbe wetu.

Kwa hivyo, neno "Tunashirikiana" linafafanua mambo yanayo tuunganisha sote na yale tunayoufanyia ulimwengu kwa ukarimu.



TUNASHIRIKIANA....

Maono ya uumbaji

Maono tunayo shirikiana ni maono ya Mungu ya upatanisho, wokovu, utimilifu, haki na Amani jinsi yanavyoelezwa katika maandiko. Shalomu inamaanisha utimilifu wa Amani. Mungu anataka sana kuimarisha agano la Amani la kudumu kati yake na binadamu pamoja na vitu vyote viliv-youmbwa.

Picha imepigwa na Jude Vickery (juu) na hakimiliki Pavel Klimenko/Adobe Stock

Mbwa mwitu ataishi pamoja na mwana kondoo, chui atapumzika pamoja na mwana-mbuzi. Ndama na simba watakula pamoja, na mtoto mdogo atawaoongoza... Katika mlima mtakatifu wa Mungu hakutakuwa na madhara wala uharibifu. Maana kumjua Mwenyezi-Mungu kutaenea pote nchini, kama vile maji yajaavyo baharini.


—*Isaya 11:6-9*

Maono ya Mungu ya Amani kuhusu vitu vilivyoumbwa yalidhihirishwa wazi katika maisha , kifo, na kufufuka kwa Yesu Kristo, aliyetangaza kuja kwa ufalme wa Amani wa enzi ya Mungu hapa duniani. Injili au "Habari Njema" ilikabidhiwa kwa kanisa-jumuia ya wanafunzi walioitwa kuwa mwili wa Kristo. Lengo la kanisa ni kuwatayarisha wanafunzi wanaoshirikiana kwa uaminifu injili ya Amani ya Kristo kwa uwezo wa roho mtakatifu.

Lakini sasa, kwa kuungana na Kristo Yesu, ninyi ambao hapo awali mlikuwa mbali, mme karibishwa kupitia kwa damu ya Kristo. Maana Kristo mwenyewe ametuletea Amani kwa kuwafanya Wayahudi na watu wa mataifa mengine kuwa jamii moja. Kwa mwili wake yeye mwenyewe aliubomoa ule ukuta ulio watenganisha na kuwafanya maadui...akaja akahubiri Amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na Amani kwao wale waliokuwa karibu.

—Waefeso 2:13-14:17

Msalaba wa Kikristo na muhuri wa jumuia ya Kristo vinaonyesha na kusisitiza wajibu tulionao kwa maono ya Mungu ya haki na Amani kwa vitu vyote vilivyo umbwa. Maono hayo yalitangazwa na manabii kwa uaminifu na kudhihirishwa ndani ya Yesu Kristo, anayewaita wanafunzi wa kila umri ili waweze kushiriki katika Amani yake kote ulimwenguni.






 Picha kutoka kwa kumbukumbu za Jumuia ya Kristo (juu kushoto) na iliyopigwa na Bob Thomas (juu kulia)

TAFAKARI

• Ni vitu gani duniani unavyoviona kuwa vizuri sana au vinavyo kupa furaha?

• Ni vitu gani duniani unavyovipenda lakini vimevunjika, vimeharibika, au vinahitaji uponyaji? Kuvunjika, kuharibika, au kujeruhiwa huko kulifanyika vipi? Je, unaweza kufanya nini ili kuisaidia hali hiyo? Kanisa linaweza kufanya nini ili kusaidia hali hiyo?

• Unawezaje kueleza maana ya msalaba na muhuri wa kanisa kwa mtu ambaye hajawahi kuviona vitu hivyo? Ni vipi ambavyo ishara hizi ni muhimu kwako? Kwa nini?



TUNASHIRIKIANA....

Jina

Sisi ni Jumuia ya Kristo! Tunashirikiana jina moja kote ulimwenguni ambalo limetafsiriwa kwa lugha nyingi. Jina letu ni aminifu kwa urithi wetu na aminifu kwa kitambulisho na wito wetu katika nyakati hizi.

"Jumuia ya Kristo, jina lenu, mlio pewa kama Baraka ya kiungu, ni kitambulisho na wito wenu."

—Kanuni na Maagano 163:1

TAFAKARI

• Tafakari juu ya jina lako au majina ambayo umesikia katika maisha yako yote. Ni vipi ambavyo umeweza kutambuliwa kwa sababu ya jina lako?

• Ungejibu vipi kama mtu ange kwambia , "Jumuia ya Kristo?" sijawahi kulisikia jina hilo".

Picha (juu kulia) hakimiliki © Taiga/Adobe Stock

Comunidad de Cristo
Kihispania

Community of Christ
Kiingereza

Gemeenschap van Christus
Kiholanzi

Kristi Samfunn
Kinorweyi

Ulukuta Lwakwa Klistu
Kibemba

Kominote di Kris
Krioli

Idung Mbiowo Christ
Kiefiki

Reszturánus Egyesület
Kihungaria

Communauté du Christ
Kifaransa

Comunidade de Cristo
Kireno

Gemeinschaft Christi
Kijerumani

Содружество Христа
Kirusi


Gulu la Khristu
Kichewa

Христова Спільнота
Kiukreni

Autahi no te Metia
Kitahiti

ქრისტეს თანამეგობრობა
Kijojia





 Picha (kushoto) kutoka kwa kumbukumbu za Jumuia ya Kristo. Picha (kulia) imepigwa na David Wheaton



Siku za usoni

Tunaendelea kuwa "Jumuia ya Kristo!" Siku zetu za usoni zina uwezekano mkubwa , changamoto zinazostahili, pamoja na tumaini tunapoendelea kukubali kuongozwa na Mungu ambaye ameliongoza kanisa tangu lilipoanza.

"Jumuia ya Kristo", jina lenu, mlio pewa kama Baraka ya kiungu, ni kitambulisho na wito wenu. Mkitambua na kukubali maana kamili ya jina hilo, mtagundua siku zenu za usoni, na vile vile mtakuwa Baraka kwa vitu vyote vilivyoumbwa. Msiogope kwenda mlikoitwa".

—Kanuni na Maagano 163:1

TAFAKARI

• Ni vipi ambavyo changamoto yakuwa "Jumuia ya Kristo" inatakiwa kuwabadilisha wanaoikubali?



Amani ya Yesu Kristo

Uunuo wa Mungu kupitia kwa Yesu Kristo na uwepo unaoendelea kuwa nasi kupitia kwa Roho Mtakatifu, kama inavyoelezwa katika maandiko ni msingi wa imani, kitambulisho, misheni, ujumbe na mambo tunaaminia.

Hapo awali katika historia kanisa lilifahamu wito wa kueneza ukamilifu wa injili kote ulimwenguni (Kanuni na Maagano 1:4) na "kuleta na kudumisha kusudi la ufalme wa Mungu" (Kanuni na Maagano 6:3). Nyakati hizi, tunafahamu kwamba

Picha (juu) imepigwa na Marvin Crozier na (chini) hakimiliki Dndavis/Dreamstime

wito huo unahusu kushiriki amani ya Yesu Kristo katika viwango vya mtu binafsi, baina ya watu, jumuia na ulimwengu wote.

Kushirikiana Amani ya Yesu Kristo kuna husisha kutoa kwa ukarimu na kwa huruma ushuhuda, huduma, sakramenti, na maisha ya jumuia yanayowapatanisha na kuwarudisha watu katika uhusiano mwema na Mungu, na wao wenyewe, na wengine, na vitu vyote vilivyoumbwa. Mtazamo huu ni njia kamili ya kutangaza na kuonyesha kwamba injili ni aminifu katika kutuwezesha kufahamu mapenzi ya Mungu. Mbinu hii ndiyo maana kamilifu ya urejesho.

Mlima yaweza kutoweka, vilima vyaweza kuondolewa, lakini fadhili zangu hazitaondoka kwenu , na agano langu la amani halitaondolewa, asema Bwana akuhurumiaye.

—Isaiya 54:10

Nawaachieni amani; nawapeni amani yangu. Siwapi ninyi kama vile ulimwengu hupeanavyo.

—Yohana 14:27

Na ni nani atakayetangaza amani, hata, habari za furaha kuu, jinsi watakavyokuwa wazuri juu ya milima.

—1 Nefi 3:189

Kwa maana yeye (Yesu) ndiye amani yetu, aliyewafanya Wayahudi na watu wa mataifa mengine kuwa jamii moja. Kwa mwili wake yeye mwenyewe aliubomoa ule ukuta ulio watenganisha na kuwafanya maadui.... Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu...

—Waefeso 2:1-4, 17

Yesu Kristo ambaye ni mfano halisi wa amani ya Mungu, anawaalika watu wote waje kupokea amani ya kiungu ingawaje maishani kuna maswala magumu na kung'ang'ana. Fuateni Kristo ili muweze kupokea amani ya Mungu na kugundua Baraka zijazo kwa kupokea wokovu.

Kwa ukarimu waambieni watu juu ya mwaliko huu, huduma, na sakramenti ambazo kwazo watu wanaweza kukutana na Kristo aliye hai, anayeponya na kuwapatanisha watu kupitia kwa uhusiano wa ukombozi katika jumuia takatifu. Kuwafanya watu wawe na uhusiano mwema au wa haki na Mungu, na watu wengine, na nafsi zao, na ulimwengu kwa jumla ni kusudi la kimsingi la safari yenu kama watu wa Imani.

—Kanuni na Maagano 163:2



TAFAKARI

- Ni vipi ambavyo umepata amani ya Kristo (haki, hali njema na ukamilifu) katika maisha yako?
- Ni vipi ambavyo unaweza kushiriki na mtu mwingine amani ya Yesu Kristo?

Mbinu hii ya jumla ya kutangaza na kuonyesha injili ni aminifu kwa ufahamu wetu bora wa mapenzi ya Mungu.



Picha kutoka kwa kumbukumbu za Jumuia ya Kristo


TUNASHIRIKIANA....

Hadithi takatifu

Hadithi takatifu ni ufunuo wa matukio ya kazi ya Mungu ya upatanisho ulimwenguni. Hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ndiye anayeita wanadamu ili wawe na uhusiano naye, na pia anataka usitawi wa uumbaji wote. Ufunuo huu ulionyeshwa kwanza katika vitabu vya Biblia ya Kiebrania, hadi katika agano jipya kwa kuja kwa Yesu Kristo, Mungu ndani ya mwili wa mwanadamu.

Maktaba hii ya vitabu inaitwa Biblia inaikita kanisa katika hadithi takatifu kwa kuelimisha na kuarifu Imani, kitambulisho, na misheni ya jumuia ya Kristo kwa ulimwengu.

Kwa habari zaidi kuhusu vile tunayoifafanua hadithi takatifu inayopatikana katika maandiko, tazama kauli yenye kichwa" Maandiko katika Jumuia ya Kristo" inayopatikana katika ukurasa 25 na katika mtandao: www.CofChrist.org/scripture/



TAFAKARI


• Chukua muda wa kuyatafakari maswali yaliyo katika waraka wa "Maandiko katika Jumuia ya Kristo".

Kielelezo (juu) na Jeff Predmonte, Picha (juu kulia) imepigwa na Jack Martin

Hadithi ya kazi ya Mungu ya mgeuzo ulimwenguni haikuisha na ushuhuda ya waandishi wa Biblia. Hadithi hiyo iliendelea katika maisha na ushuhuda wa kanisa nzima la Kikristo, na pia katika sehemu zingine. Hadithi takatifu ni tukio la kitendo cha Mungu cha ukombozi ulimwenguni. Vizazi vingi vya wafuasi wengi wa Kikristo wameandika sura zingine katika hadithi hii inayoendelea. Hadithi takatifu inayopatikana katika maandiko na katika desturi kuu ya Kikristo, inaimarisha na kuelimisha ufahamu wetu na wito wetu. Kitambulisho chetu cha pekee kinahusu hali ya kudai nafsi yetu katika kikundi kikubwa cha Wakristo ambao kila wakati na kila mahali wanamuita Yesu Kristo. Sisi pamoja nao, tunaendelea kuandika sura mpya katika hadithi hiyo ya zamani ya Yesu Kristo na upendo wake.

Msisahau kusikiliza kwa makini kuhadithiwa kwa hadithi takatifu, kwani hadithi ya maandiko na Imani uwezesha na kuangaza.

—Kanuni na Maagano 161:5



Picha imepigwa na John Weese

Hadithi ya Jumuia ya Kristo ni sehemu ya hadithi kuu takatifu iliyo na mizizi yake katika historia ya Kikristo, ikiwemo tamaduni ya Kiebrania iliyoibua Ukristo. Katika historia hiyo kuu Jumuia ya Kristo ina hadithi fulani inayotia moyo, iliyo maridadi na ya kimataifa. Kanisa ilianza katika miaka ya mwanzo ya 1800 katika sehemu ya kaskazini ya New York, Marekani, wakati wa uhuwishaji wa Kikristo. Kufikia sasa, kanisa liko katika mataifa yanayokaribia 50.

Hadithi ya kanisa ni ya imani isiyo ya kawaida, maono, na ubunifu katika kuitikia wito wa Mungu. Tunamwona Roho wa Mungu akitenda kazi katika kila kitambulisho cha hadithi ya imani yetu. Kitendo kilichoanza kwa kijana fulani kumtafuta Mungu kwa njia ya maombi katika miaka ya mwanzo wa 1800 kinaendelea hadi sasa. Mungu hukipa kila kizazi tambuzi, uzoefu, na changamoto kwa ajili ya makusudi ya kiungu.



Picha hakimiliki Siloto/Adobe Stock

Uraisi wa kwanza umeweza kutoa kanuni za historia ya kanisa za kusaidia kuongoza kanisa kuendelea kuchunguza historia yake. Kanuni hizo zimetolewa katika utambuzi wa viongozi wa zamani na wa sasa wa kanisa la ulimwengu mzima, wanahistoria wa kanisa, wanateolojia, na wengine wengi.

Kwa taarifa kamili ya mitazamo kuhusu historia ya kanisa "tazama ukurasa wa 76 au soma katika mtandao www.CofChrist.org/church-history-principles



Historia ya Jumuia ya Kristo ni sehemu ya historia takatifu kubwa zaidi ambayo ina mizizi yake katika historia ya kikristo.

TAFAKARI

Baada ya kuchunguza "mitazamo kuhusu historia ya kanisa" jibu maswali yafuatayo:

- Kuna tofauti gani kati ya kuitazama historia kama kitu "kilichotendeka" na "mtazamo wa mtu kuhusu kilichotendeka?" Je, kunaweza kuwa na kitu kinachojulikana kama "historia rasmi?"

- Chagua mtu mmoja, kikundi, au enzi katika historia ya kanisa. Ufahamu wako umebadilika vipi baada ya kupata mtazamo au habari zaidi? Mbona mara nyingi hali hii huwa ngumu kushughulikiwa?

- Unadhani washirika wa siku za usoni wataionaje Jumuia ya Kristo katika miaka ya mwanzo wa karne ya 21? Unaweza kufanya nini nini wakati huu ili kuwasaidia kuelewa kinachoendelea kanisani au katika jamii?



TUNASHIRIKIANA....

Misheni

Tnawezaje kushiriki amani ya Yesu katika viwango vya mtu binafsi, baina ya watu, jumuia na ulimwengu wote?

Kauli ya misheni ya kanisa la ulimwengu nzima inatuonyesha njia ya kufanya hivyo:

Tunatangaza Yesu Kristo na kukuza Jumuia za furaha, tumaini, upendo, na amani.



Tunatangaza Yesu Kristo!

Tunatangaza Yesu Kristo kwa kueneza injili mahali tunapoishi na kote ulimwenguni, pamoja na huduma ya kuwakaribisha watu, ushuhuda, ushirika, ibada, utunzaji na uundaji wa uanafunzi wa nyakati zote.

Kauli ya Jumuia ya Kristo kuhusu Kristo inayosema "Tunatangaza Yesu Kristo" inapatikana katika ukurasa wa 58 au katika kiungo cha mtandao www.CofChrist.org/ we-proclaim-jesus-christ.

Tunakuza Jumuia!

Tunakuza jumuia za nchi na za ulimwengu wote zinazodhihirisha utawala wa Mungu wa amani duniani. Katika sehemu zingine za ulimwengu, hili linajulikana kama kusudi la tumaini la ufalme wa Mungu.

Tunapotangaza Yesu Kristo kwa njia ifaayo kwa kushiriki ushuhuda wetu, huduma, na sakramenti, na kukuza jumuia za haki na amani zinazomzingatia Kristo, basi tunashiriki amani ya Yesu Kristo.

 Picha (juu na juu) imepigwa na Wayne Rowe

Misheni ya Yesu Kristo Ni misheni yetu

Misheni ya Yesu Kristo ndio muhimu Zaidi katika safari iliyo mbele.

—Kanuni na Maagano 164:9f

Katika Luka 4:18-19, Yesu alitangaza misheni au utume wake aliposoma kutoka kwa maandishi ya Isaya:

"Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiria maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa".

Yesu ametiwa mafuta kwa misheni takatifu:

- Uinjilisti: Kutumwa kutangaza habari njema na kuwaalika wengine wajiunge naye katika misheni.
- Huduma zenye huruma: Zinazofikia waliovunjika moyo, wanaoteseka, na wale wanaohitaji tumaini na amani ya Kristo.
- Haki na kufanya amani: Kuwaachilia wale walioshikwa mateka na mifumo isiyo ya haki na mazingira ya maisha ambayo yanashusha thamani ya mtu yeyote.

Ufalme ulikuwepo katika huduma ya Kristo kama ilivyoelezwa katika Matendo ya Mitume. Waumini hao wa kwanza waliendeleza utume wa Kristo kwa kumtangaza Kristo aliye hai, akiwaalika watu wote katika jamii, wakithamini thamani ya kila mtu, kwa ukarimu na kwa huruma kukidhi mahitaji yao na kutafuta haki na amani kwa kila mtu.



Picha imepigwa na Wayne Rowe

Mipango 5 za Misheni Zote ni muhimu!

Wito wetu ni kurudisha maono yale yale na shauku kwa utume wote wa Yesu Kristo kupitia njia tano za kubadilisha maisha, kubadilisha kanisa na mabadiliko ya kimisheni ya ulimwengu.



Alika watu kwa Kristo

Misheni ya Kristo ya uinjilisti

Tumejiandaa kushiriki amani ya Yesu Kristo na wale ambao wanangojea kusikia maneno y ukombozi ya injili.

Kumaliza umaskini, na mateso

Misheni ya Kristo ya huruma



 Picha imepigwa na Wayne Rowe

Tumejiandaa kuwa mikono na miguu ya Kristo, tukifikia huduma za huruma ambazo zinahudumia maskini na wenye njaa na kuzuia hali zinazopunguza thamani ya watu.

Fuata amani duniani

Ujumbe wa misheni ya Kristo wa haki na amani

Tumejiaandaa kurejesha agano la Kristo la amani, hata Sayuni ya matumaini yetu. Tumaini la Sayuni litakuwa kweli wakati tunapoishi amani ya Kristo na kushiriki amani yake na wengine.



Kukuza wanafunzi wa kutumika

Wape vifaa watu binafsi kwa misheni ya Kristo

Tumejiaandaa kuwapa wanaume, wanawake, na watoto kuwa kweli na vielelezo hai ya maisha, huduma, na kuendelea kwa uwepo wa Kristo ulimwenguni.

Kuzoea makongamano katika misheni

Wape makusanyiko vifaa vya kufanya misheni ya Kristo

Tumejiaandaa kuwa makongamano ambayo ni ya kweli, na yaliyo vielelezo hai vya Yesu Kristo, tukiunganishwa na Roho Mtakatifu, na kutumwa ulimwenguni kama mashahidi wa Kiuinjilisti, wahudumu wenye huruma, na haki na wapatanishi.

Tutakuwa watu wa kinabii wenye sifa ya kujitolea kwa kawaida kwa huruma na amani ya Mungu iliyo funuliwa katika Yesu Kristo.

Misheni za Kristo... misheni zetu

Sala ya misheni:

Mungu, Roho yako itatuongoza wapi leo?

Nisaidie kuwa Macho kabisa na kuwa tayari kujibu.

Nipe ujasiri wa kuhatarisha kitu kipya na kuwa Baraka ya upendo wako na amani.

Amina

TAFAKARI

- Je! Utaitikiaje wito wa Mungu wa kuweka maisha yako katika misheni takatifu ya mwaliko, huduma ya huruma, na haki na kufanya amani?
- Tunawaambia wengine juu ya Yesu Kristo kwa kushiriki kwa ukarimu, ushuhuda wetu, rasilimali, na msaada. Je! Ni kwa njia gani kongamano lako, kituo cha misheni, na huduma ya kibinafsi huwaambia wengine kuhusu Yesu Kristo?
- Fikiria mtu mmoja ambaye maisha yake yangebadilishwa sana na ujumbe wa injili ya Kristo. Ni kwa njia gani unaweza kushiriki ujumbe huo?





Tunapomtangaza Yesu Kristo kwa kushiriki shuhuda zetu, huduma zetu, sakramenti zetu, na kukuza jumuia za haki na amani inayozingatia Kristo, tunashiriki amani ya Yesu Kristo.



Picha imepigwa na Wayne Rowe

Kanuni za Kudumu na mambo ya msingi ya Imani

Kuna uhusiano gani kati ya kanuni za kudumu na mambo ya msingi ya Imani? Watu wanapojaribu kuelewa kitambulisho, misheni, na ujumbe wa kanisa, wao huchangia kuweko kwa njia mbalimbali za kuutazama ukweli, na jambo hilo husababisha maswali mbalimbali.

Kanisa liko katika hali gani? Kanuni za kudumu ni ukweli na thibitisho za msingi zinazounda sifa ya Kanisa. Kanuni za kudumu zinatoa miongozo ya jinsi ya kuishi katika jumuia, familia, mahali pa kazi, kusanyiko, utamaduni wetu. Zinafafanua vile tunapata na kushirikiana injili na kanisa pamoja na watu wengine.

Kanisa linaamini nini? Mambo ya msingi ya Imani ni ufafanuzi mpana wakimantiki kuhusu kile ambacho kanisa linashikilia kuwa kweli, na mambo hayo yamepangwa katika makundi yaliyo sehemu ya desturi pana ya Kikristo. Mambo ya msingi ya imani yanawakilisha kiwango cha kina cha uchunguzi kuhusu injili na kanisa.

Tunahitaji njia zote mbili za kueleza kitambulisho, misheni, na ujumbe wa kanisa, pamoja na njia zingine zilizoelezwa katika waraka huu, ili kuhakikisha kwamba watu wanaweza kuchunguza na kuipata injili kwa njia bora zinazoweza kuwapa habari na pia kuwageuza.



TUNASHIRIKIANA....

Kanuni za kudumu



Msingi: Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu

Ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo na uwepo wa kudumu wa Roho Mtakatifu, unaoelezwa katika maandiko, ni msingi wa Imani yetu, kitambulisho, misheni, ujumbe , na mambo ya msingi ya Imani.

Kwa kuitikia kwa uaminifu urithi wetu na uzoefu wa kudumu na Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu, tunajitahidi kuthibitisha kanuni za kudumu zifuatazo (maadili, mawazo, maudhui) kama sehemu muhimu ya kitambulisho na misheni ya kanisa. Kanuni za kudumu zinafafanua asili, kiini, au nafsi ya kitambulisho, misheni, na ujumbe wa kanisa. Zinaeleza sifa za kanisa kama zinavyooneshwa katika washirika, kusanyiko, na mashirika yanayoshirikiana na kanisa kote ulimwenguni.

Picha zimepigwa na Bob Thomas





Watu wengine huziita kanuni za kudumu "maadili ya kiini". Wengine huziita "mawazo ya kimsingi". Tumia maneno yanayoleta maana inayofaa katika mazingira unayoandikia ndani, unayoshiriki, unayofunza, au unayo hubiri ndani. Kwa makusudi rasmi ya jumla, kanisa la ulimwengu mzima litatumia maneno haya "kanuni za kudumu".

Kanuni za Kudumu

Kila kanuni inafuatwa na kauli zinazosaidia kueleza maana yake. Kila kikundi cha kauli kinamalizia kwa kauli za "tu" zinazosisitiza wito na kitendo kinachotakikana. Kauli zinazofuata kila kanuni hazitakiwi kuwa kikomo au za kutosha. Zimetolewa kama njia ya kuweza kusaidia. Tumia sentensi fupi, picha, hadithi, ushuhuda, vifungu vya maandiko, na vidokezo vingine kueleza wazi na kuwafahamisha watu unaoshirikiana nao.

Neema na ukarimu

- Neema ya Mungu iliyofunuliwa katika Yesu Kristo, ni karimu na haina masharti.
- Baada ya kuipokea neema ya Mungu ya ukarimu tunatoa kwa ukarimu na kupokea kwa neema ukarimu wa wengine.
- Tunajitoa kikamilifu na kutoa vyote tulivyonavyo kwa kusudi la Mungu kama ilivyo funuliwa katika Yesu Kristo.
- Tunashirikiana kwa ukarimu ushuhuda, mali, huduma, sakramenti zetu kulingana na uwezo wetu.

Utakatifu wa Uumbaji

- Hapo mwanzo, Mungu aliumba vitu vyote na akasema kila kitu alichoumba kilikuwa nzuri.
- Roho na vitu vya asili, vinavyo onekana na visivyo onekana, vinahusiana.
- Nguvu za uumbaji za kuumba au kuharibu inatukumbusha kwamba tunaweza kudhuriwa katika maisha haya.

Picha hakimiliki Chaiyon021/Adobe Stock (juu kushoto) na zimepigwa na Jude Vickery (juu kulia)

- Mungu anaendelea kuumba kwa ajili ya kutimiza kusudi la kiungu.
- Tunajiunga na Mungu kuwa watumishi wa kutunza na kuleta tumaini kwa vitu vyote vilivyo umbwa.

Ufunuo unaoendelea

- Maandiko ni ushuhuda wa ufunuo na ni ya msingi katika kuitikia kwa mwanadamu ufunuo wa mungu wenye hali ya kiungu.
- Mungu hutufunulia kwa neema mapenzi yake ya kiungu wakati huu kama alivyofanya katika nyakati zilizopita.
- Roho Mtakatifu hutoa ufunuo na kutoa ushuhuda kuhusu ukweli wa kiungu.
- Kwa unyenyekevu, kila mtu na pia jumuia nzima husikiliza kwa hali ya maombi ili tuweze kuyafahamu kikamilifu mapenzi ya mungu kuhusu maisha yetu, maisha ya kanisa, na ya uumbaji.

Thamani ya kila mtu

- Mungu anawaona watu wote kuwa na thamani kubwa iliyo sawa.
- Mungu anawataka watu wote waweze kuwa na ukamilifu wa mwili, akili, roho, na uhusiano.
- Tunajitahidi kutetea na kurudisha thamani ya watu wote kwa mtu binafsi na katika jumuia, k wa kuipinga mifumo isiyo ya haki, inayo punguza thamani ya binadamu.
- Tunaungana na Yesu Kristo kupeleka habari njema kwa maskini, wagonjwa, wafungwa na wanaoteseka.



Picha imepigwa na John Weese

Watu wote wameitwa

- Mungu huwapa watu vipawa na nafasi kwa neema ili waweze kutenda matendo mema na kushiriki katika makusudi ya mungu.
- Yesu Kristo hualika watu wamfuate kwa kuwa wanafunzi wanao shiriki katika uzima na huduma yake.
- Wanafunzi wengine wameitwa na kutawazwa kufanya majukumu fulani ya ukuhani kwa ajili ya jumuia, kusanyiko, na ulimwengu.
- Tunaitikia kwa uaminifu, kwa kusaidiwa na Roho Mtakatifu, kadiri ya ufahamu wetu wa wito wa mungu.



Chaguo la kuajibika

- Mungu huwapa binadamu uwezo wa kufanya chaguo kuhusu nani au nini watakachotumikia.
- Watu wengine hupitia hali zinazo punguza uwezo wao wakufanya chaguo.
- Chaguo wanalofanya wanadamu huchangia wema au uovu katika maisha yetu na katika ulimwengu.
- Hali nyingi za uumbaji zinahitaji ukombozi kwa sababu ya chaguo baya na la dhambi linalofanywa na binadamu.

Tumeitwa ili kufanya chaguo jema katika hali za maisha yetu zinazochangia makusudi ya Mungu.

Kuandama Amani (Shalomu)

- Mungu anaitakia Uumbaji wote amani (haki, upatanisho, uzima, ukamilifu, na amani).
- Yesu Kristo ambaye ni mfano halisi wa amani ya Mungu, anayefunua maana ya amani ya Mungu katika hali zote za maisha.
- Maono ya ufalme wa Mungu ni kukuza utawala wa Mungu duniani, kama inavyotangazwa na Yesu Kristo, kupitia kwa ushawishi inayo geuza ya jumuiya zenye haki na amani.
- Tunashirikiana na wengine amani ya Yesu Kristo kwa Ujasiri na ukarimu.
- Kwa kuongozwa na Roho Mtaka-

Picha imepigwa na Wayne Rowe



tifu, tunafanya kazi na Mungu pamoja na watu wengine, ili kurudisha amani kwa uumbaji.

- Tunasherehekea amani ya Mungu popote inapotokea au inapoandamwa na watu wenye nia njema.

Umoja katika utofauti

- Jumuia ya Kristo ni familia ya kimataifa, yenye wanafunzi, watafutaji, na kusanyiko tofauti tofauti.
- Huduma za nchi na za ulimwengu mzima zinategemeana na ni muhimu kwa misheni ya kanisa.
- Dhehebu linatambua u tofauti na umoja kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu.
- Tunajitahidi kuwa na maafikiano au makubaliano ya yote katika maswala muhimu. Iwapo hatuwezi kupata maafikiano tutaendelea kujadiliana na kuunga mkono kwa upendo, Imani yetu ya pamoja na misheni ya kanisa.
- Tunakiri kwamba kutokuwepo kwa maafikiano kati yetu katika maswala fulani kuna waumiza baadhi ya watoto wapendwa wa Mungu na Uumbaji.

Baraka za jumuia

- Injili ya Yesu Kristo hudhihirishwa Vyema katika maisha ya jumuia ambapo watu huweza kuhatarika na neema ya Mungu na vilevile kuathiriana.
- Jumuia ya kweli inahusisha huruma na mshikamano na watu walio maskini, wanaotengwa, na wanaoteswa.
- Jumuia ya kweli hutetea thamani ya kila mtu na vilevile hutoa mbadala unaofaa kwa kujipenda mno, kukaa upweke, na ukubalifu.
- Jumuia takatifu hutoa nafasi za mafunzo na ustawi kwa watu wote, hasa kwa wale wasioweza kujitunza kikamilifu.
- Tunathamini uhusiano wetu. Tunashirikiana hali kuu ya kuaminiana na kuwa kitu kimoja – hata kama hatujawahi kukutana.
- Wanafunzi wengine wameitwa na kutawazwa kufanya majukumu fulani ya ukuhani kwa ajili ya jumuia, kusanyiko, na ulimwengu.

- Tumeitwa ili kuunda jumuiya za amani ya Kristo katika familia na kusanyiko zetu na katika vijiji, makabila, mataifa, na hata uumbaji wote.

Ili kuona vile washirika wa kanisa kote ulimwenguni hudhihirisha kanuni za kudumu, tazama kauli hii: "Sisi ni kitu kimoja, Sisi ni wengi" katika ukurasa 68.


TAFAKARI

- Chagua kanuni ya kudumu moja au Zaidi inayo kunenea. Soma waraka wote wa "Sisi ni kitu kimoja, Sisi ni wengi" na uone vile kanuni hiyo imedhihirishwa.

- Andika, tafakari, au jadili na mtu mwingine, vile umeiona kanuni hiyo ikidhihirishwa katika maisha yako, huduma yako, au kusanyiko lenu.




Picha imepigwa na Wayne Rowe



TUNASHIRIKIANA....

Mambo ya Msingi





Mambo ya Msingi ya Imani ya Jumuia ya Kristo

Dibaji

Habari njema ya Yesu Kristo ni kiini cha Imani na mambo ya msingi ya Imani ya Jumuia ya Kristo. Sisi ni jumuia ya ulimwengu wote na tume-jitolea kumfuata Yesu, kuleta ufalme wa Mungu duniani, na kuungana pamoja kutafuta uwepo wa Roho Mtakatifu unaotoa ufunuo na kutu-tia nguvu. Tunawasilisha mambo ya msingi ya Imani yetu, si kwamba ni neno la mwisho, bali ni mwaliko ulio wazi wa kuanza safari ya uanafunzi. Tunapotafuta ushauri wa Mungu wa kudumu, tunawahimiza watu wote wajifunze maandiko na kufikiria juu ya uzoefu wao wanaposhiriki katika maisha ya kanisa.

Mungu

Tunamwamini Mungu mmoja aishie, anayekutana nasi kupitia kwa ushuhuda wa Israeli, anaye-funuliwa ndani ya Yesu Kristo, na anayetembea katika uumbaji wote

Kielelezo hakimiliki Vadimsadovski, Picha hakimiliki (juu) Ricardoreitmeyer na (chini) Brian Jackson/Adobe Stock

kama Roho Mtakatifu. Tunakiri utatu-Mungu aliye katika nafsi tatu. Vitu vyote vinavyoishi viliumbwa na Mungu: fumbo lisiloweza kufahamika na upendo unaopita mawazo. Mungu huyu pekee ndiye anastahili ibada yetu.

Yesu Kristo

Tunamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aishie, neno aliyefanyika mwanadamu, mwokozi wa ulimwengu, mwanadamu kamili na mungu kamili. Kupitia kwa maisha na huduma, kifo na kufufuka kwa Yesu, Mungu hupatanisha ulimwengu na kuzivunja kuta zinazotenganisha watu. Kristo ni amani yetu. Tazama kauli ya "Kisitolojia" –"Tunatangaza Yesu Kristo" ukurasa wa 58 na katika mtandao wa kanisa www.CofChrist.org/ we-proclaim-jesus -christ.

Roho Mtakatifu

Tunamwamini Roho Mtakatifu, mtoa uzima, hekima takatifu, Mungu wa kweli. Roho anayetembea katika uumbaji na kuudumisha; analiweka kanisa wakfu kwa ajili ya misheni, anauweka ulimwengu huru kutokana na dhambi, udhalimu, na kifo; na kuwageuza wanafunzi. Popote tunapopata upendo, amani uvumilivu, wema, ukarimu, uaminifu, upole, na kiasi, Roho Mtakatifu anafanya kazi mahali hapo.

Uumbaji

Kama dhihirisho la upendo wa Mungu, Mungu aliumba mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo, na kuviita"vyema". Kila kitu kinamilikiwa na Mungu na kinatakiwa kutunzwa na kutumiwa kwa haki kulingana na makusudi ya kiungu. Mungu anauona uumbaji kama kitu kizima bila kutenganisha Roho na vitu vya asilia. Mungu anawahitaji watu wa kila kizazi wajiunge naye kuwa watumishi wa kuutunza uumbaji kwa upendo.

Mwanadamu

Kila mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Mungu aliuchukua udhaifu na desturi ya mwanadamu kupitia kwa Yesu Kristo, naye anajulikana kupitia kwa vitu hivyo. Kwa hivyo, tunakiri bila kinzano thamani ya kila binadamu. Pia tunakiri kwamba Mungu amewabariki wanadamu na kipawa cha nguvu: uwezo wa kuchagua utatumikia nani au nini katika hali zetu za maisha.

Dhambi

Mungu alituumba ili tuwe njia ya kuonyesha upendo na wema. Ilhali sisi huzitumia vibaya nguvu zetu binafsi na kwa jumla. Sisi huchukua vipawa vya uumbaji na vipawa vyetu wenyewe na kuvigeuza kinyume cha makusudi ya Mungu na kupata matokeo ya kuhuzunisha. Dhambi ni hali ya ulimwengu wote kufarakana na kutenganishwa na Mungu na pia kutengana kati yetu wenyewe. Tunahitaji neema ya kiungu hiyo peke yake hutupatanisha na Mungu na pia kuwa na upatanisho kati yetu wenyewe.

Wokovu

Injili ni habari njema ya wokovu kupitia kwa Yesu Kristo: msamaha wa dhambi, uponyaji wa hali za utenganisho, kuvunjika, na nguvu za vurugu na mauti. Uponyaji huu ni wa mtu binafsi, mashirika ya wanadamu, na uumbaji wote. Uzima huu mpya ni kipawa cha upendo cha neema ya Mungu tunachopewa kupitia kwa Imani na toba. Ubatizo ni njia ya kudhihirisha kujitolea kwetu kuwa wanafunziwa siku zote. Tunapotoa maisha yetu kwa Kristo katika ubatizo, tunaingia katika jumuia ya Wakristo (mwili wa Kristo) na tunapata ahadi ya wokovu. Tunapata wokovu kupitia kwa Yesu Kristo, lakini tunakiri kwamba neema ya Mungu haina mpaka na upendo wa Mungu ni mkuu kuliko ufahamu wetu.

Kanisa

Mungu anakusudia Imani ya Kikristo iweze kudumishwa kwa kuungana na Yesu Kristo na wanafunzi wengine ili kuhudumia



Picha imepigwa na Wayne Rowe

ulimwengu. Kanisa la Yesu Kristo lina watu walioitikia wito wa Yesu. Jumuia ya Kristo ni sehemu ya mwili wa Kristo. Tumeitwa kuwa watu wa unabii, tunatangaza amani ya Yesu Kristo, na kuunda jumuia ambazo watu wote watakaribishwa na wataweza kuwa na uhusiano mpya na Mungu, ambapo hakutakuwa na maskini.

Ufunuo

Tunakiri kwamba Mungu aishie anaendelea kujidhihirisha kwetu. Mungu amefunuliwa kwa ulimwengu kupitia kwa ushuhuda wa Israel, na Zaidi ya hayo kupitia kwa Yesu Kristo. Kupitia kwa Roho Mtakatifu tunaendelea kumsikia Mungu akinena nasi katika nyakati hizi. Kanisa linahitajika kuungana pamoja kusikiliza kile ambacho Roho anasema kisha kuitikia kwa uaminifu.



Maandiko

Maandiko ni maandishi yaliyofunuliwa na Roho wa Mungu na kukubaliwa na kanisa kama dhihirisho sanifu la kitambulisho, ujumbe, na misheni ya kanisa. Tunakiri kwamba Biblia ni maandiko ya kimsingi ya kanisa. Pia, jumuia ya Kristo inatumia Kanuni na Maagano-sio kuchukua nafasi ya Biblia au kuiboresha, lakini ni kwa sababu inathibitisha ujumbe wa Biblia kwamba Yesu Kristo ni neno hai la Mungu. Maandiko yakitumiwa vyema na kwa uaminifu, hutoa ushahuri wa kiungu na ujuzi uliofunuliwa kwa ajili ya uanafunzi wetu. Tazama kauli hii "maandiko katika Jumuia ya Kristo" katika ukurasa wa 63 na katika mtandao www.CofChrist.org/scripture-in-community-of-christ.

Sakramenti

Sakramenti ni huduma maalum ambazo kanisa imepewa kwa ajili ya



 Picha zimepigwa na Bob Thomas (juu kushoto) na Jack Martin (juu kulia)

kuwasilisha neema ya Yesu Kristo kwa wafuasi wake na kwa watu wote ambao anataka kuwagusa kwa huruma yake. Sakramenti hizi ni ubatizo, uthibitisho, meza ya Bwana, ndoa, kuwabariki watoto, kuwawekea wagonjwa mikono, na baraka ya mwinjilisti. Katika huduma hizi, Mungu huitakasa vitu vya kawaida vya uumbaji ili kuyabariki maisha ya wanadamu na kuyafanya kuwa mapya na kulifanya kanisa kutafuta ufalme wa Mungu wa amani. Tazama kiungo cha mtandao www.CofChrist.org/sacraments.

Uanafunzi

Kuwa Mkristo sio tu kuwa na orodha ya mawazo sahihi; bali ni kumtii Yesu kikamilifu katika kila hali ya maisha. Upendo wa Mungu usio na mipaka hutuweka huru ili tuishi maisha ya wakala wazuri natuweze kutoa maisha yetu kwa ukarimu kumtumikia Mungu. Uanafunzi ni safari ya ndani na nje. Yesu hutuita tumfuate na pia kuwakaribisha wengine ili waweze kupata kujua nguvu za neema yake zinazogeuza.

Huduma

Huduma ni utumishi wa unyenyekevu unaotolewa kwa kufuata mfano wa Yesu, anayemwita kila mwanafunzi aweze kushiriki katika kazi ya kuhudumia ulimwengu. Wanafunzi wengine wameitwa na Mungu na wametawazwa katika vyeo vya ukuhani ili waweze kutekeleza misheni ya kanisa kwa njia maalum. Roho mtakatifu huwapa wanafunzi wote vipawa na uwezo wa kukamilishana ili mwili wa Kristo uweze kutayarishwa kuwa ushahidi ulimwenguni.

Utawala wa Mungu

Utawala wa Mungu ni ushindi ujao wa upendo, haki, fadhili na amani, ambao siku moja uta ukumbatia uumbaji wote. Maisha na huduma ya Yesu ni dhihirisho la ahadi hiyo. Aliwafunza wanafunzi wake kuomba ili ufalme wake uje kwa ukamilifu na akawatuma ulimwenguni ili waweze kuwa ishara ya uumbaji huo mpya. "Ufalme wa Mungu" unaonyesha kujitolea kwetu kuutangaza ufalme wa Mungu wa amani duniani kwa kuunda jumuia zinazomzingatia Kristo katika familia, kusanyiko, makazi ya watu, mijini, na kote ulimwenguni.

Amani

Amani ya Mungu ni haki, uadilifu, uzima na ustawi wa uumbaji wote. Yesu, Mfalme wa amani, alikuja kuhubiri ufalme na pia kuwa amani yetu kupitia kwa msalaba. Roho Mtakatifu hutupa uwezo wa kuandama amani na haki kwa watu wote.

Ufufuo na uzima wa milele

Kristo amefufuka! Tunaamini kwamba Mungu, ni Mungu wa uzima, bali si wa mauti. Kwa Imani tunashirikiana katika uzima wa milele hata sasa. Katika Kristo, upendo wa Mungu utashinda kila kitu kinachodharau na kuishusha hadhi ya

uumbaji hata kifo chenyewe. Pasaka hutupa tumaini kwamba mateso na mauti yaliyowapata waathiriwa katika historia, si jambo la mwisho. Tunamwamini kwamba Roho Mtakatifu ataigeuza uumbaji wote ili uweze kushiriki katika utukufu wa Mungu.

Hukumu

Mungu aishie ambaye tunatumikia ni Mungu wa haki na fadhili. Mungu hujali tunavyo wafanyia majirani na maadui zetu na vile tunavyo tumia vipawa vya uumbaji. Inajalisha Mungu sana vile tunavyo wakaribisha masikini, wageni, wagonjwa, wafungwa, na waliokataliwa. Tunakiri kulingana na maandiko kwamba Yesu Kristo ni wakili na hakimu wa watu walio hai na waliokufa.

Siku ya mwisho

Tunaendelea kumtumikia Mungu tukijua kwamba kazi yetu si bure. Uumbaji wa baadaye ni wa Mfalme wa Amani, sio wa watu wanaodhulumu, wanaoamuru, au wanaoharibu. Tunapotarajia kuona siku za usoni, tunajitahidi kutafuta amani ya Kristo na kuiandama. Hatujui siku wala saa ya kuja kwake Kristo bali tunajua kwamba Mungu ni mwaminifu. Tukimwamini Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu, tunatarajia kuziona siku za usoni tukiwa na tumaini, tukiomba ombi aliyetufunza Yesu kuomba: "Ufalme wako uje! Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko Mbinguni."

TAFAKARI

- Fikiria vile ufahamu wako kuhusu mambo ya msingi ya Imani unafanana au unatofautiana na mambo yaliyotajwa hapa.
- Fikiria vile ungeweza kueleza mambo haya ya Imani kwa mtu anayetafuta kufahamu mambo ya msingi ya Imani kuhusu Jumuia ya Kristo.



TUNASHIRIKIANA....

Uwakili wa maisha yote

Uwakili ni jibu la watu wangu kwa huduma ya mtoto wangu na inahitajika sawa na wale wote wanao tafuta kujenga ufalme.

—Kanuni na Maagano 147:5a

Kuishi maisha kwa ukarimu

Yote tuliyo na yote tuliyo nayo ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Tunatafuta kushiriki kwa ukarimu kile tulichopokea kama kitendo cha imani na shukrani kwa yote ambayo mungu ametupatia. Tukiwa na Yesu Kristo kama kielelezo chetu, tumeitwa kutumia wakati, vipawa vyetu vyote wakati wetu, talanta, hazina na huduma ya ushuhuda wa Mungu na wengine.

Ili kuwa wakarimu kwa ajili wa wengine, ni lazima tukawe katika uwezo wetu wakushiriki zawadi zetu kutoka kwa Mungu. Ukarimu wa Mungu unapo tubadilisha, tunataka kutumia maisha yetu kuwatumikia wengine.

Tunahudumu kupitia zaka ya wakati wetu, talanta, hazina, na ushuhuda. Tunaelezea hii kama uwakili huu wa maisha yote. Kuwa mawakili wazuri wa maisha yetu ndiyo wito wetu wa mwisho kama wanafunzi wakarimu.

Picha (juu) imepigwa na Martin Crozier

Kutoka kwa kile mtu ambaye amepewa mengi, mengi yatatakiwa: na kutoka kwa yule ambaye amepewa dhamana kubwa, hata Zaidi itahitajika.

—Luka 12:48

Zaka ni nini?

Zaka ni mazoea ya kiroho ambayo yanaonyesha utayari wa kutoa kila mwelekeo wa maisha ya mtu kwa Mungu.

—Kanuni na Maagano 165:2d

Maneno haya yanapojitokeza kanisani uthibitisho, ufuatao unatuongoza:

Uwakili ni mwitikio wa maisha yote kwa neema ya Mungu na huduma ya Yesu Kristo. Njia moja ya uwakili inadhihirishwa ni kupitia mazoezi ya kiroho ya kutoa zaka. Ingawa zaka inamaanisha sehemu ya kumi, kutoa kwa ukarimu uwezo wako wa kweli ni roho ya kutoa zaka.

Utoaji zaka ya wakati, talanta, hazina, na ushuhuda huunga mkono huduma za kanisa za mitaa na za ulimwengu ili kutekeleza misheni ya Yesu Kristo.

Wanafunzi wote wameitwa kama mawakili waaminifu wanaotoa zaka.

—Maamuzi ya ushauri wa kanisa la Ulimwengu 1314



Jibu la ukarimu la mwanafunzi

Kanuni sita za majibu ya ukarimu ya mwanafunzi inatuongoza katika kusimamia na kugawana rasilimali zetu kwa sababu ya kusudi la Mungu. Ikiwa tutatumia kanuni hizi kwa maisha yetu, tuta jifunza kuoanisha vipaumbele vyetu na vipaumbele vya Mungu, na mioyo yetu na moyo wa Mungu.

Pokea zawadi za Mungu

Kanuni 1. Mungu anawazawadisha kila mtu kwa neema isiyo na mipaka na upendo usio kuwa na mwisho. Zawadi za Mungu kwa kila mmoja wetu zinaonyeshwa kupitia maisha na huduma ya Yesu Kristo.

TAFAKARI

• Je! Unahisi ukarimu wa Mungu maishani mwako?

Jibu kwa uaminifu

Kanuni 2. Tunapojibu kwa uaminifu huduma ya Yesu Kristo tunawajibika kwa mtu mwingine, Mungu, na sisi wenyewe. Jibu letu kwa zawadi za Mungu za upendo na neema ni kuwatumikia wengine na kuruhusu ukarimu uwe sehemu ya maumbile yetu.

TAFAKARI

• Nini kinacho kuchochea kuwa mwaminifu?

Oanisha moyo na pesa

Kanuni 3. Kusimamia pesa tulizo nazo. Haijalishi ni kiasi gani, Inadhihirisha hamu yetu ya kumpenda na Kumsaidia Mungu, majirani, sisi wenyewe, na Ulimwengu. Tunapozingatia utoaji wetu kwa makusudi ya Mungu, mioyo yetu inaoanishwa zaidi na moyo wa Mungu.

TAFAKARI

• Ikiwa mtu angeangalia jinsi unavyotumia pesa zako, wangeweza kuhitimisha nini juu ya moyo wako?

Shiriki kwa ukarimu

Kanuni 4. Kutoa zaka ni zoezi la kiroho. Ni zawadi ya shukrani kwa Mungu kwa zawadi za ukarimu za Mungu kwetu sisi. Tunapo shirikiana zaka zetu, kanisa linaweza kueneza furaha, tumaini, upendo, na amani ulimwenguni ili wengine pia waweze kupata ukarimu wa Mungu.

TAFAKARI

• Nini kimechochea kutoa katika hatua mbali mbali za maisha yako: mtoto, ujana, mtu mzima na mtu mzima aliyekomaa?

Weka akiba kwa busara

Kanuni 5. Kuweka akiba ni njia ya kujiandaa kwa siku za usoni. Inatupa nafasi ya kupanua upendo wetu na kuunda kesho bora kwa familia zetu, marafiki, misheni ya kanisa na ulimwengu.

TAFAKARI

• Je! Ni mifano gani ya hali inayo tarajiwa na isiyo tarajiwa ambayo unaweza kuweka akiba?

Tumia kwa uajibikaji

Kanuni 6. Matumizi ya kuajibika ni kujitolea kuishi maisha yenye afya, furaha, pamoja na Mungu na wengine. Mafundisho ya Yesu yanatupa changamoto ya kuchagua mtindo wa maisha ambao mara nyingi ni kinyume na tamaduni.

TAFAKARI

• Jinsi gani unapata usawa sawa kati ya mahitaji na matakwa.

Wanafunzi waaminifu huitikia ufahamu unaozidi kuongezeka wa ukarimu tele wa Mungu kwa kushiriki kulingana na matakwa ya mioyo yao... toa kwa ukarimu kulingana na uwezo wako wa kweli.

—Kanuni na Maagano 163:9

Fungua uwezo kamili wa misheni ya Kristo kupitia ukarimu ambao unaiga ukarimu wa Mungu.

—Kanuni na Maagano 165:2a

TAFAKARI

• Wewe binafsi au kama jumuiya, unaigaje ukarimu wa Mungu?



Picha imepigwa na Tignor

Kuguswa na ukarimu wa Mungu

Mwaliko

Maisha yetu yanapoguswa sana na Mungu, tunataka kuwa kama Kristo maishani mwetu. Sisi kama wanafunzi wa Yesu Kristo tunatambua neema ya Mungu na upendo wake katika maisha yetu. Kukubali zawadi za Mungu inamaanisha kutoa maisha yetu yote kwa Kristo kama mwanafunzi mwaminifu.

Umealikwa kwenye safari uwakili wa maisha yote kwa kuitikia ukarimu wa kushangaza wa Mungu maishani mwako tunapotafuta kujenga jumuiya za furaha, tumaini, upendo, na amani. Fungua uwezo kamili ya misheni ya Kristo kupitia ukarimu ambao unaiga ukarimu wa Mungu.

—Kanuni na Maagano 165:2a



Picha imepigwa na Paul Davis



TUNASHIRIKIANA....

Sakramenti

Aangalia hasa sakramenti ili kuimarisha maisha ya Kiroho ya mwili.

—Kanuni na Maagano 158:11c

Kwa ukarimu shiriki mwaliko, huduma, na sakramenti ambazo watu wanaweza kukutana na Kristo aliye hai ambaye huponya na kupatanisha kupitia uhusiano wa ukombozi katika jamii takatifu.

—Kanuni na Maagano 163:2b

Sakramenti

Tunakutana na Mungu kupitia Sakramenti za kanisa, ambazo zinagusa maisha katika nyakati na mahali muhimu. Sakramenti huleta neema ya Mungu, ushawishi wa Roho Mtakatifu, na mfano wa maisha ya Yesu Kristo pamoja na kujitolea kwa mtu binafsi kwa Imani. Kupitia Sakramenti, tunagundua uwepo wa Mungu kila mahali na tunatambua kuwa maisha yote ni matakatifu. Kukutana huku kunaelekeza hamu ya upendo wa Mungu wa kuleta watu wote kwa Imani, utimilifu, na uhusiano mzuri kati yao na Mungu, ambayo ndio maana ya wokovu.

Sakramenti huburudisha, hufanya upya na inatupa changamoto ya kuendelea na misheni ya Kristo, misheni yetu, kwa ajili ya uumbaji wote.

Jumuia ya Kristo ina Sakramenti nane, nyingi ambazo zinaadhimishwa katika uzoefu wa ibada kwa nyakati zinazofaa.

Ubatizo

Yesu alianza kazi yake kwa kuomba abatizwe. (Mathayo 3: 13-17). Ubatizo ni kitendo cha hadharani kutangaza kuwa unachagua kumfuata Yesu Kristo kwa moyo wako wote, nguvu, akili na nguvu zote. Ni uamuzi ambao unaashiria hatua muhimu katika kutambua mpango wa Mungu maishani mwako, kumgeukia Mungu, na kuingia kwenye uhusiano wa agano na jumuia ya wanafunzi na Mungu.

Katika ubatizo, tuna zamishwa ndani ya maji kuashiria kifo katika dhambi na kuinuliwa kutoka kwa maji kuanza maisha mapya. Paulo, aliyebadilishwa mapema kuwa

 Picha imepigwa na Marvin Crozier

Mkristo, aliandika jinsi ubatizo unavyoashiria kufuata kamili kwa Yesu na mabadiliko makuu ya maisha: "Wakati mlizikwa pamoja naye katika ubatizo, mlifufuliwa pamoja naye kwa njia ya imani katika uwezo wa Mungu" (Wakolosai 2:12).

Uthibitisho

Wakati Yesu alitoka majini (Mathayo 3:13-17), Roho Mtakatifu iliwakilishwa kama njiwa, ilishuka juu yake. Kama wafuasi wa Yesu Kristo, tunabatizwa kwa maji na Roho Mtakatifu. Kufuatia ubatizo wa maji, wanafunzi wapya hushiriki sakramenti ya uthibitisho. Ina "thibitisha" ushirika katika Jumuia ya Kristo, na inathibitisha baraka ya Roho Mtakatifu inayoendelea kwa kila mwanafunzi.

Katika Sakramenti ya uthibitisho, wazee huweka mikono juu ya kichwa cha mwanafunzi mpya, na mzee mmoja hutoa sala maalum. Sala ya uthibitisho hutafuta baraka za Mungu kusaidia washirika wapya kukua katika agano lao na kushiriki kwa ukarimu karama zao kuunga mkono misheni ya kanisa. Kujitolea iliyofanywa kupitia ubatizo na uthibitisho ni changamfu" uanafunzi ulidhihirishwa kupitia agano na Mungu na wengine katika jamii takatifu."

Kanuni na Maagano 164:2d. Uthibitisho husaidia kuunganisha watu pamoja katika jamii-kusanyiko na kanisa la ulimwengu ili waweze kukua katika uanafunzi.

UBATIZO



UTHIBITISHO



Meza ya Bwana

Yesu aliwapa wanafunzi wake kipande cha mkate na kinywaji cha divai na akawaambia: "twaeni, huu ni mwili wangu...hii ni damu yangu ya agano, inayomwagwa kwa ajili ya wengi" (Marko 14:22-24).

Injili ya Luka inazidi kusema, "Fanyeni hivi kwa kunikumbuka" (Luka 22:19). Meza ya Bwana inashirikishwa Jumapili ya kwanza ya kila mwezi katika kongamano na hafla maalum.

Wote wamwaminiae Kristo, ambao kawaida huonyeshwa katika ubatizo wa maji iwe ni washiriki wa Jumuia ya Kristo au la, wanakaribishwa kushiriki meza ya Bwana. Hii ni fursa ya kusherehekea tena maagano yetu ya ubatizo na uthibitisho, kupa

MEZA YA BWANA



Tunakutana na Mungu kwa njia ya sakramenti za kanisa, zinazogusa maisha katika nyakati na mahali muhimu.

tanisha uhusiano, na kujitolea tena kwa misheni ya kanisa. Inachukua jukumu muhimu katika uponyaji na kuimarisha kongamano la jamii. Matayarisho yanapaswa kujumuisha kupatanishwa na wengine, kukiri makosa yetu, na kumuomba Mungu msamaha. Hatuwezi kupatanishwa na Mungu ikiwa hatuja patanishwa na wengine (Mathayo 5:23-24).

Kutawazwa


Yesu aliwaita watu wamfuate, na wawe wanafunzi wake, na watumie karama zao kwa wengine (Luka 6:12-13). Wengine wameitwa na Mungu kuwa wahudumu wakutawazwa kwa sababu karama zao zinawasaidia kutumikia jamii ya agano kwa njia maalum.

Kutawazwa kunatambua mpango wa kiungu wa kuwaita wanafunzi Fulani kwa majukumu na huduma za ukuhani kwa sababu ya jamii, kusanyiko na hata ulimwengu. Sakramenti hii mara nyingi hufanywa katika ibada takatifu. Mawaziri wanaofanya kazi, kawaida wawili, huweka mikono yao juu ya kichwa cha mtu huyo. Waziri mmoja hutoa sala, akitaja ofisi maalum ya ukuhani ambayo mtu huyo anatawazwa, na inaweza kujumuisha mwongozo wa baraka. Kusanyiko, linalowakilisha kanisa lote hujitolea kupokea huduma ambayo itatoka kwa mshiriki mpya wa ukuhani.

Kutawaza hupeana mamlaka kwa washiriki wa ukuhani kulingana na majukumu makuu ya ofisi zao za ukuhani. Washiriki wa ukuhani



KUTAWAZWA



utenda ndani ya miongozo na mazingira ya jamii ya kanisa, wakishikilia viwango vya juu vya maadili ya huduma na kutumikia kwa uadilifu na uaminifu.

Baraka za watoto

Wakati Yesu alikuwa mtoto mdogo, Mariamu na Yusufu walimchukua na kumpeleka hekaluni" ili wampeane kwa Mungu" (Luka 2:2135). Wakati wa huduma ya Yesu ya watu wazima, wazazi walileta watoto wao kwake ili wabarikiwe (Marko 10:14). Wakati familia zinawaleta watoto wao kubarikiwa na wazee, wanaitikia neema ya Mungu kwa kuchagua kumlea mtoto wao katika jamii yenye upendo wa Mungu na kuahidi kutoa mwongozo na malezi katika maisha yote ya mtoto. Kongamano hujitolea kuwa jamii yenye upendo ambayo mtoto anaweza kufanikiwa na kuwa kama mwanafunzi wa Yesu Kristo.

Wazee wawili husimamia Baraka za watoto, kawaida wakati wa ibada mbele ya familia ya mtoto na kusanyiko. Wazee hushikilia, huunga mkono au kuweka mikono yao juu ya mtoto, na mzee mmoja hutoa sala ya Baraka. Watoto kutoka watoto wachanga mpaka umri wa miaka 7 wanaweza kubarikiwa. Sakramenti hii inapatikana kwa mtoto yeyote bila kujali ushirika wa familia katika Jumuia ya Kristo.

Kuweka mikono kwa wagonjwa

Yesu aliwabariki wale ambao walikuwa wanaumia kwa njia nyingi. Wanafunzi waliwapaka mafuta wengi waliokuwa wagonjwa na kuwaponya. (Marko 6:13). Tunapata hadithi nyingi za kuwabariki wagonjwa katika agano jipya, zinazoonyesha tamanio la Mungu la ukamilifu na Shalomu kwa viumbe vyote.

BARAKA ZA WATOTO



KUWEKA MIKONO KWA WAGONJWA



Wakati wa shida ya mwili, akili au hisia watu wanaweza kutafuta sakramenti hii kutoka kwa wahudumu. Sakramenti hii inafungua njia ya uponyaji kwa njia yoyote itakayokuja.

Kawaida wazee wawili husimamia Sakramenti hii pamoja. Wanamtembelea mtu huyo ilikujua Zaidi hitaji la mtu huyo. Mzee mmoja huweka tone la mafuta yaliyowekwa wakfu kwenye paji la uso la mtu huyo, huweka mikono juu ya kichwa cha mtu huyo na kutoa taarifa ya kusudi na Baraka. Kisha mzee wa pili anaweka mikono juu ya kichwa cha mtu huyo na kutoa sala ya utimilifu na ustawi. Hii inaweza kufanywa faraghani au mbele ya familia, marafiki na katika kusanyiko. Sakramenti hii inapatikana kwa wote wanaotafuta ukamilifu katika mwili, akili na roho.

Ndoa

Yesu Kristo alifundisha kwamba dhamana kati ya watu wawili wanaopendana na kujitolea kwa kila mmoja katika agano rasmi ni takatifu. (Matayo 19:4-6). Alibariki ndoa kwa uwepo wake (Yohana 2:1-11). Ndoa ya Kikristo ni agano takatifu kati ya watu wawili kwa urafiki wa maisha, afya, na upendo. Ndoa pia ni makubaliano ya kisheria. Sakramenti ya ndoa inaonyesha tamanio la Mungu la kutia nguvu na kuimarisha ndoa. Sherehe ya ndoa katika Jumuiya ya Kristo inajumuisha taarifa ya agano la pande zote, "Ninyi wawili mnakubali kuwa mwenzi wa kila mmoja"... (Kanuni na Maagano 11:2b), na sala ya tamko, "Mungu aongeze Baraka zake na akuhifadhi" kutimiza maagano yako tangu sasa na hata milele". Amina. (Kanuni na Maagano 111:2d)

NDOA



Picha hakimiliki Jana Marie Photography

Makubaliano ya wanandoa yanaanzisha dhamana ya maisha yote, agano la kushiriki upendo kama Wakristo wao kwa wao, na wengine, na Mungu. Makuhani pamoja na wazee wa Jumuia ya Kristo wanaweza kufanya Sakramenti hii, bila kujali ushirika wa wana ndoa katika Jumuia ya Kristo maadamu sheria za mitaa zinazoongoza ndio zinafuatwa.

Baraka za Kiinjilisti

Yesu aliomba ombi maalum kwa wanafunzi wake kuwaongoza katika safari yao (Yohana 17, Luka 22:31-32). Leo, Baraka za Kiuinjilisti inaweza kuombwa na watu binafsi, wanandoa, familia, kaya, vikundi, na makutano ambao wanataka kuhisi neema na mwongozo wa upendo wa Mungu. Wakati hutumika katika kujiandaa kupitia maombi, mazoezi ya Kiroho, kusoma, na utambuzi. Mwinjilisti au timu ya wainjilisti wataongoza maandalizi. Mara baada ya maandalizi kukamilika mwinjilisti au wainjilisti hutoa sala.


Sakramenti hii ina hashiria upendo wa Mungu wa ulimwengu kwa mpokeaji au wapokeaji na inaleta hakikisho, inafafanua chaguzi, na hutoa mwangaza kwa ufuasi wa uaminifu kwa kuitikia Mungu.

BARAKA ZA KIINJILISTI



TUNASHIRIKIANA....

Hekalu kama Ishara ya kutoa uzima





Sisi kama Jumuia ya Imani tumepewa vipawa vingi, maandiko, sakramenti, ujuzi wa kiroho, na ishara zinazo tufanya tuelekeze maisha yetu kwa Kristo ili tuweze kuimarisha uhusiano wetu wa Imani. Miongoni mwa Vipawa hivi ni hekalu iliyo kule Kirtland (Ohio, Marekani) na nyingine iliyo Independence (Missouri, Marekani). Hekalu hizo mbili zilizo jengwa kwa ufundi wa hali ya juu sana inatuita ili tuwe na heshima kuu na kustaajabu tunapoona uzuri huo unazozifana nafsi zote zihitaji kumwabudu Mungu aliye muumba na mdumishaji wa vitu vyote. Tukiwa ndani ya hekalu hizo hatuwezi kuzama katika mawazo yetu wenyewe na kujikweza.

Hekalu hizo mbili iliyo Kirtland na vilevile Independence – inatukumbusha kwamba, Zaidi ya mambo yote, Yesu Kristo anataka kuturudisha katika maisha tuliyotakiwa kuishi alipotuumba; maisha ambayo Mungu alikusudia; maisha yaliyo na upendo, ukarimu, mahusiano ya pande mbili, kushirikiana na amani.

Picha zimepigwa David Wheaton (juu) Picha kutoka kwa kumbukumbu za Jumuia ya Kristo (kati na chini)




Hekalu hizo, mahali pa uzuri, ibada, elimu, na uongozi wa kanisa ni dira na mnara wa taa unaongoza safari yetu ya Imani. Inatumika kutukumbusha kila mara kwamba tunatakiwa kuishi kinyume cha tamaduni za kutenga, ubinafsi, tamaa, na tuhuma zinazotuzingira. Hekalu hizo hutuelekeza kwa wito wetu wa kweli wa kuwa jengo la Mungu la Kiroho, lililojengwa juu ya msingi wa ushuhuda na dhabihu ya Yesu Kristo – Makao yanayo unganisha, yanayoponya, yanayorudisha, na kuwaeka watu huru kupitia kwa jumuia ili waweze kutenda mambo kwa njia bora zaidi bila kujali hao ni kina nani... makao ambayo Yesu atajihisi yuko nyumbani! (Maneno haya yametolewa katika ujumbe aliyotoa Steve Veazey tarehe 10 Juni, 2007 wakati wa ibada ya kusherekea uwekaji wakfu cha kituo cha hekalu cha Kirtland cha wageni na uundaji wa mambo ya Kiroho.)

Jipangeni:

> *Tayarisheni kila kitu kinachohitajika na uanzishwe nyumba, nyumba ya maombi, nyumba ya kufunga kula, nyumba ya Imani, nyumba ya kujifunzia, nyumba ya utukufu, nyumba ya mpango, nyumba ya Mungu; ili kuingia kwenu katika nyumba hiyo iwe katika jina la Bwana; na kuondoka kwenu katika nyumba hiyo kuwe katika jina la Bwana.*
>
> —Kanuni na Maagano 85:36 b-c

Hekalu itatumika kuandama amani. Itatumiwa kufanya shughuli za upatanisho na uponyaji wa roho. Pia itatumiwa kufanya shughuli za uimarishaji wa Imani na matayarisho ya ushuhuda. Kutokana na huduma hiyo mwenendo wa ukamilifu wa mwili, akili, na roho kama lengo linalotarajiwa utaimarishwa. Itakuwa njia ya kutoa mafunzo ya uongozi



Mahekalu, maeneo ya uzuri, ibada, elimu, na mwongozo wa kanisa, ni dira na taa kwa safari yetu ya Imani.

kwa makuhani na washirika nayo (Hekalu) itakuwa mahali ambapo maana muhimu ya Urejesho, kama njia ya uponyaji na ukombozi itapewa uzima na ufahamu mpya unaopewa msukumo na uzima na ushuhuda wa Mkombozi wa ulimwengu.

—Kanuni na Maagano 156:5e

Acheni (Hekalu) isimame kama ishara inayosimama wima ya watu waliokabiliana na udhalimu na ugomvi mipakani na ambao sasa wanatafuta amani ya Yesu Kristo kote ulimwenguni.

—Kanuni na Maagano 161:2b

Muwe watu wa Hekalu-wanaoona vurugu lakini wanatangaza amani-wanaohisi ugomvi lakini wananyosha mkono wa upatanisho, wanaokabiliwa na roho zilizovunjika lakini wanapata njia ya uponyaji.

—Kanuni na Maagano 161:2a


...hekalu huita kanisa zima kuwa patakatifu pa amani ya Kristo, ambapo watu kutoka mataifa yote, makabila, na hali za maisha wanaweza kukusanywa katika makao ya kiroho bila kugawanya kuta, kama utimizo wa maono ambayo Yesu Kristo alidhabihu maisha yake.

—Kanuni na Maagano 163:8c

Ndani yake jengo lote linaunganishwa vyema na kukua hata liwe Hekalu takatifu katika Bwana; ndani yake ninyi nanyi mwajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.

—Waefeso 2:21-22

Ishara ya Hekalu iliyo na mzunguko na inayomzingatia Kristo na makusudi yake yaliyofafanuliwa inadhihirisha kiini cha uwepo wa Mungu ulio pamoja nasi. Picha na mawazo hayo vinatumika kulifanya kanisa lizingatie kitambu-





lisho, ujumbe, na misheni yake ya kweli. Tunapokua watu wa Hekalu, tuta ongozwa kukubali mambo "yaliyo muhimu sana" katika uzima wa kanisa. Kusema kweli-athari ya Hekalu iliyopo sasa ingekosekana hatungeweza kuyazingatia mambo yafuatayo kama tunavyofanya sasa:

- Hitaji la kumwendea Mungu kwa heshima kuu na kwa njia ya ajabu katika enzi hii ya kushuku.
- Maono ya Mungu ya amani kwa vitu vilivyoumbwa.
- Uhusiano wa kadiri ya ulimwengu wakihalisia na wa kiroho.
- Amani, upatanisho, na uponyaji wa roho ni sifa muhimu sana katika huduma ya Yesu Kristo.
- Uzima wa mwili, akili, na roho.
- kama hali inayotakiwa kwa wote.
- Maana muhimu ya urejesho kama njia ya uponyaji na ukombozi.
- Safari ya siku zote ya ndani na ya nje ya mwanafunzi, kama inavyofafanuliwa na ishara ya Hekalu.
- Wito wa kanisa wa "andama amani" na kuwa "kimbilio la amani ya Kristo" kote ulimwenguni.
- Wito wa kushiriki katika uhusiano wa muungano baina ya Imani mbalimbali kwa sababu Hekalu ni nyumba ya maombi kwa kila Imani.

Timu ya Hekalu ya mkakati imeifafanua kiini cha Hekalu kuwa:

 Picha zimepigwa na Dave Wheaton

Urudishaji wa Shalomu ya Mungu: Safari ya mgeuzo ya mtu binafsi na ya jumuia

Wazo na lugha ya Shalomu inateka vizuri msingi bora wa jumla na wa kimaandiko kuhusu huduma zinazoambatana na ishara na makusudi ya Hekalu. Safari ya Kikristo ni hija inayoongoza kuifikia Shalomu; mwendo unaoongoza katika ukamilifu uliofunuliwa kwa njia ya Kristo. Maisha, huduma, kifo na ufufuo wa Yesu unaotuingiza katika uhusiano wa moyoni na Mungu na kutusababisha kufanya kazi ya misheni; kujumuisha ukamilifu na neema katika ulimwengu unaoteseka. Yesu ndiye "njia". Yesu mwenyewe ndiye safari ya Kikristo, hija inatuwezesha kumfikia Mungu. Hekalu inaashiria Mungu akiwaita watu waende katika hija. Safari hiyo ni muhimu. Sisi ni watu walio katika hija ya kumwendea Mungu na kuufikia ulimwengu wa Mungu. Huo ndio mfuatano wa mambo ya kila siku katika uanafunzi tunao alikwa kuingia ndani. Tunaposafiri, tunafanya agano ya kuwa "maskani ya Mungu" (Waefeso 2:22). Sisi tunataka kuwa "Hekalu ya amani ya Mungu" kwa ajili ya familia, marafiki, kusanyiko, jumuia, dhehebu,, ulimwengu na utawala wa Mungu.

Tunaunga mkono kusudi la kuirudisha Shalomu ya Mungu kwa kuunganisha nidhamu ya ibada, uundaji, na desturi ili kusababisha mgeuzo.



Picha imepigwa na Wheaton

Ibada

Maana... mtaongozwa kwa lmani.

—Isaya 55:12

Acheni Hekalu iendelee kujidhihirisha kama kituo kitakatifu cha ibada, elimu, ujenzi wa jumuia, na matayarisho ya wanafunzi.

—Kanuni na Maagano 163:8b

Uundaji

Kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani.

—Luka 1:79

Mungu anaitaka Jumuia ya kinabii kuibuka kutoka katika mataifa yote ya ulimwengu, jumuia yenye sifa za kujitolea kwa hali isiyo ya kawaida kwa huruma na amani ya Mungu iliyofunuliwa kupitia kwa Yesu Kristo.

—Kanuni na Maagano 163:11a

Desturi

(hali inayorejea ya kitendo cha kugeuza na tafakari)

Tafuta amani na kuizingatia.

—Zaburi 34:14

Kukutana na muumba na mpatanishi wa milele kunakogeuza kuna wangoja wanafuata njia za kiroho za (Hekalu) za uponyaji, upatanisho, amani, uimarishaji wa lmani, na maarifa.

—Kanuni na Maagano 163:8a

TAFAKARI

• Iwapo umewahi kutembelea Hekalu iliyoko Independence au Kirtland, ni vipi ambavyo tukio hilo la kuwa katika Hekalu limeathiri hali yako ya kuitikia wito wa Mungu maishani mwako? Iwapo hujawahi kuitembelea Hekalu hiyo, kumekuwa na matokeo gani maishani mwako baada ya wewe kusoma au kusikia hadithi za Hekalu kutoka kwa watu ambao wamewahi kwenda huko?

• Je, Kwako wewe, Hekalu inaashiria nini? Jambo hili linahusiana vipi na uanafunzi wako?

• Kitengo cha 163:8c kinasema hivi "Hekalu linaita Kanisa nzima liwe mahali patakatifu pa amani ya Kristo" Fikiria vile wewe binafsi pamoja na kusanyiko lenu mnafanya kazi kama mahali patakatifu pa amani ya Kristo. Unatakiwa kufanya nini kama mwanafunzi wa Kikristo ili nafsi yako iweze kuwa mahali patakatifu pa amani?





Picha imepigwa na David Wheaton



TUNAMTANGAZA YESU KRISTO

Yesu Kristo

Dibaji

Katika nyakati zote za Historia, Wakristo wamekuwa wakiieleza imani yao ndani ya Yesu Kristo. Kidesturi makanisa yametumia kauli za Imani na kukiri kwa Imani ili kueleza kwa ufasaha ufahamu wa Yesu Kristo na kazi yake. Kauli za aina hiyo zimetoa misingi muhimu ya kuwafunza wanafunzi na pia kuyajibu maswali ya Kitheolojia yanayotokea mara kwa mara.

Ingawa maneno hayawezi kutosheleza kikamilifu, kauli ifuatayo inaeleza kiini cha mambo ya imani ya Jumuia ya Kristo. Hatutarajii kwamba kila mtu ataikubali kauli hii na pia kukataa matumizi ya kauli hii. Lakini ombi letu ni kwamba kanisa litaona taarifa hii kuwa muhtasari wa kuvutia wa imani yetu, na kwamba muhtasari huu utaweza kutoa usaidizi katika kuitekeleza misheni ya kanisa kwa kutangaza Yesu Kristo na kukuza jumuia za furaha, tumaini, upendo na amani.

1. Sisi kama washirika wa Jumuia ya Kristo, tume unganishwa na Wakristo walio kila mahali na wa nyakati zote kwa kumkiri Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, mwanzilishi wa wokovu wetu, na kichwa cha kanisa.
2. Yesu Kristo ni neno aliyefanyika mwili, yeye ni mwanadamu kamili na Mungu kamili. Ndani yake tunajiona sisi wenyewe na pia tunamwona Mungu ambaye Yesu alimwita Baba, mwenye huruma, aliyeumba vitu vyote na akatangaza kwamba kila kitu kilikuwa "kizuri sana". Yeye na Roho Mtakatifu ni kitu kimoja.
3. Kupitia kwa muujiza wa kupata mwili, Yesu alizaliwa na Mariamu, akaja duniani kuishi na kukaa miongoni mwetu ili kutufunulia hali na mapenzi ya Mungu. Kwa hali ya kinabii aliushutumu udhalimu katika Hekalu na kutangaza Habari Njema ya kuja kwa utawala

Picha (juu) hakimiliki Kovalenko/Adobe Stock

wa Mungu hapa duniani, akatangaza kuwekwa huru kwa wanaoteswa na toba kwa watesaji. Aliwafunza wafuasi wake kumpenda Mungu, kuwapenda jirani zao, kuwapenda adui zao. Yesu alitangaza kwamba watu wote wana thamani kubwa machoni pa Mungu alipofanya matendo yafuatayo: kula na watenda dhambi, kuwatumikia masikini, kuwaponya wagonjwa, kuwabariki watoto na kuwakaribisha wanawake na wanaume kuwa sawa miongoni mwa wanafunzi wake.


4. Yesu alisalitiwa na rafiki zake, alishitakiwa kwa kukufuru na kufanya kitendo cha uhaini, akahukumiwa na Pilato, kufa msalabani, na akasulubiwa katikati ya wezi wawili waliokuwa waalifu. Kwa kuwasamehe watu waliomwua na kuamua kuchukua dhambi, uchungu, mateso ya ulimwengu mzima, aliwa patanisha wanadamu wote na Mungu.
5. Siku ya tatu, alifufuka kutoka kwa wafu, akathibitisha maisha yake na huduma yake, akaushinda udhalimu wote, pamoja na kifo. Akapaa mbinguni, baada ya kuwapa wafuasi wake mamlaka ya kuhudumu katika jina lake, duniani kote. Alimtuma Roho Mtakatifu awe nao wanaposhuhudia habari njema ya ufufuo.
6. Kristo ni amani yetu, kwani amezivunja kuta za uhasama zilizokuwa katikati yetu. Anatuahidi ukombozi na uponyaji wa uhusiano kati yetu na Mungu, kati yetu wenyewe, na kati yetu na uumbaji wote.



Uchongaji uliofanywa na Guiseppe Runggaldier. Iliyopeanwa kwa hekalu iliyoko Independence na kusanyiko la Jenkinton, PA mwaka wa 2006. Picha imepigwa na Martin

7. Kanisa ambalo ni mwili wa Kristo, limeitwa ili iweze kutangaza injili mpaka Kristo atakaporudi tena. Yeye ndiye anaye tusamehe katika ubatizo, na utulisha mezani pake. Sisi kama wanafunzi wa Kristo, tumeitwa ili tuweze kuishi maisha yanayokubaliana na ya Yesu kwa kuishi katika jumuia za kuwapenda wengine, kumwona Yesu ndani ya nyuso za watoto wa Mungu, na kuwahudumia watu waliosahauliwa na ulimwengu. Tunatangaza uaminifu wetu kwa Kristo na kwa injili yake kwani yeye ndiye atakaye hukumu watu.
8. Ahadi za Mungu kupitia kwa Yesu Kristo ni za kweli-kwamba kupitia kwa Roho Mtakatifu tutapewa neema ya kutenda mambo tulio ambiwa: tutakuwa na ujasiri katika kupigania haki, hamu ya kuwa na amani miongoni mwa vurugu, msamaha wa dhambi zetu, utumishi badala ya tamaa ya vitu vya dunia, uponyaji wa mwili na Roho mahali ambapo kuna majeraha, na uzima wa milele katika kifo.
9. Tunaishi na kutumika tukiwa na tumaini kwamba ufalme wa Mungu wa haki na amani utakuja, na utauponya uumbaji wote unaokoroma. Tukiweka tumaini letu ndani ya Kristo aliyefufuka, aliye ndani yetu kupitia kwa Roho Mtakatifu, tutaendelea na safari pamoja, tukipeana Baraka, heshima na utukufu sasa na hata milele.

Kuiga kaburi ambalo Yesu alilazwa baada ya kusulubiwa.



 Picha hakimiliki Gtenda Powers/Adobe Stock

Maswali ya kutafakari na kujadiliwa na Watu Binafsi na Makundi

1. Kwa hali ya maombi soma kauli hiyo yote. Maoni yako ni yapi kuhusu mambo uliyosoma? Ni sehemu gani ina kufurahisha sana?
2. Isome dibaji kwa makini. Ni kitu gani kinasemwa kuhusu wajibu wa kauli inayomhusu Yesu Kristo-katika maisha ya kila mshirika, kusanyiko, na katika kanisa lote kwa jumla?
3. Katika aya ya kwanza, nini maana ya "tuna unganishwa... kwa kumkiri Yesu Kristo"? Je, unahisi kuunganishwa vipi na Wakristo wengine, ndani ya Jumuia ya Kristo na katika madhehebu mengine? Maneno haya –"Mwana wa Mungu aishie, mwanzilishi wa wokovu wetu, na kichwa cha kanisa"-yana maana gani kwa maisha yako binafsi na kusanyiko lenu?
4. Soma Yohana 1:1-14 ni vipi ambavyo aya ya pili inaonyesha kile ambacho mwandishi wa andiko hili anasema? Tofauti ni zipi? Yesu ana wezaje kuwa "mwanadamu kamili na vilevile Mungu kamili" bila hali moja kuipunguza nyingine? Ni vipi ambavyo Imani yako katika utatu imeonyeshwa kikamilifu katika aya hii?
5. Ni nini ambacho Yesu anatufunulia kuhusu "kuhusu hali na mapenzi ya Mungu" (Aya ya 3)? Je, huduma gani ya Yesu iliyoelezwa katika aya hii ni muhimu sana kulingana na ufahamu wako wa Mungu?
6. Ufahamu wako ni upi kuhusu wajibu wa Yesu katika kuwapatanisha "wanadamu wote kwa Mungu" (Aya ya 4)? Toa mifano ya vile wewe na watu wengine pia humsaliti Yesu siku hizi? Kwa nini msamaha ni muhimu sana katika upatanisho?
7. Nafasi ya thibitisho hili "Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu" (Aya ya 5) katika imani yako na mambo uaminio? Ni vipi ambavyo ufufuo wa Yesu ulikuwa thibitisho la maisha na huduma yake? Ni vipi ambavyo unahisi kwamba umepewa mamlaka ya kuhudumu katika jina la Yesu? Ni vipi ambavyo Roho Mtakatifu hukusaidia kushuhudia na kuhudumu?

8. Ni vipi ambavyo Kristo ni "Amani yetu" (Aya ya 6)? Ni vipi ambavyo Kristo ameleta amani maishani mwako? Je, ni uhusiano gani katika maisha yako inahitaji kuponywa?
9. Nini maana ya kulifahamu kanisa kama "Mwili wa Kristo" (Aya ya 7)? Soma 1 Wakorintho 12;12-27 ili uweze kuyaona maono ya Paulo kulihusu jambo hili. Ni nini maana ya "Kuyapatanisha" maisha yako na ya Yesu? Jambo hili itakuhitaji uya ache mambo gani?
10. Ni "Ahadi zipi za Mungu katika Kristo" (Aya ya 8) zilizo muhimu sana kwako? Unaweza kuongeza ahadi zipi katika orodha hii? Ni vipi ambavyo ahadi za Mungu ni za manufaa kwetu binafsikwa upande mmoja na kwa watu wa jumuia kwa upande mwingine?
11. Ni nini maana ya wewe "Kuishi na kutumika kwa kuwa na tumaini la ufalme wa Mungu" (Aya ya 9) Ni vipi ambavyo wewe "Unamwamini Kristo aliyefufuka?" Ni vipi ambavyo maisha yako yanaweza kumpa Mungu Baraka, heshima, na utukufu?
12. Soma tena kauli inayomhusu Yesu Kristo. Ni vipi ambavyo kutafakari kwako kuhusu dhihirisho la maisha na huduma ya Yesu imekusaidia kujitayarisha kuwa mwanafunzi bora kama mshirika wa Jumuia ya Kristo? Unawezaje kuitumia kauli hii kuwashuhudia wengine kuhusu Yesu Kristo?



 Picha hakimiliki Kovgabor 79/Adobe Stock

MAANDIKO KATIKA JUMUIA YA KRISTO

Dibaji

Maandiko yakifafanuliwa kwa njia ya kuwajibika na kutumiwa kwa uaminifu, hutoa mwongozo wa kiungu na ujuzi wa ufunuo kwa maisha. Maandiko hutusaidia kumuamini Yesu Kristo. Ushuhuda wake huongoza kwa uzima wa milele na kutuwezesha kukua kiroho, kubadilisha maisha yetu, na kujihusisha vilivyo katika maisha na uzima wa huduma ya kanisa.



Thibitisho la Kwanza

Tunatangaza kwamba Yesu Kristo-aliyeishi, akasulubishwa, akafufuliwa kutoka kwa wafu, na atakayerudi tena-ni Neno la Mungu lililo hai. Maandiko yanamlenga Yesu Kristo. Tuna uzima kupitia kwa Yesu Kristo (Yohana 5:39-40). Tunatakiwa kumsikiliza Kristo (Marko 9:7).

Thibitisho la Pili

Tunapata Neno lililo hai katika maandiko. Maandiko ni ushuhuda wa msingi wa ujumbe wa kuokoa na kubadilisha ambao Mungu amelikabidhi kanisa. Kanisa iliunda vitabu vya maandiko vinavyotambulika ili kila mara liwe na njia ya kusikia Habari Njema, kulea imani yake, kupima maisha yake, kujaribu uzoefu wake, na kukumbuka kitambulisho chake.

Thibitisho la Tatu

Maandiko ni maktaba ya vitabu vinavyozungumza kwa sauti nyingi. Vitabu hivyo viliandikwa katika nyakati na mahali mbalimbali, na

Picha hakimiliki (juu) Gino Santa Maria na (kushoto) Magdalena Kucova/Adobe Stock

hudhihirisha lugha, desturi, na hali ambazo vitabu hivyo viliandikwa. Ufunuo wa Mungu kupitia kwa maandiko ahuji kwetu isipokuwa kutoka kwa waandishi wanadamu, lakini ndani na kupitia kwa mwanadamu huyo. Katika vyombo vya udongo vya maandiko tumepewa hazina ya upendo na neema ya kiungu (2 Wakorintho 4:7).

Thibitisho la Nne

Mamlaka ya Maandiko yanapatikana kutoka kwa mfano wa Kristo, aliyekuja kuwa mtumishi (Marko 10:45). Kwa hivyo mamlaka ya maandiko si mamlaka ya kudhulumu, kutawala, au kuamuru. Ikiwa Yesu alikuja kuhudumu, kwa jinsi gani zaidi vitabu vinavyo mlenga vinatakiwa kutumiwa kama mtumishi wa makusudi ya Mungu wa kuokoa.

Thibitisho la Tano

Maandiko ni muhimu na ya msingi kwa kanisa, lakini si kwa sababu hayana makosa (kusema kwamba kila kitu ni sahihi kihistoria au kisayansi). Maandiko hayadai kuwa hivyo. Bali, vizazi vya Wakristo vimegundua kwamba maandiko ni ya kutegemewa kwa ajili ya kuwadumisha katika ufunuo, kwa kukuza imani katika Kristo, na kuyalea maisha ya wanafunzi. Bila shaka, maandiko yanaweza kutegemewa kwa makusudi hayo (2 Timotheo 3:16-17).

Thibitisho la Sita

Imani, uzoefu, desturi, na elimu ni mambo yaliyo na sehemu ya kuchangia ufahamu wetu wa maandiko. Katika kung'ang'ana ili kusikia au kuitikia ushuhuda wa maandiko,



Picha imepigwa na John Wight



kanisa linatakiwa kuthamini mwangaza unaotokana na asili hiyo.

Thibitisho la Saba

Kanisa linapojaribu kufafanua maandiko kwa njia ya kuwajibika, linahitaji msaada wa Roho Mtakatifu. Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu ataongoza wanafunzi wake kujua ukweli mpya (Yohana 16:12-15). Kupitia kwa Roho Mtakatifu, maneno ya zamani ya maandiko yanaweza kuwa ufunuo; utwezesha kupata jambo ambalo halikuweza kuonekana au kusikika hapo zamani.

Thibitisho la Nane

Wanafunzi wanatakiwa kukua katika maarifa na ufahamu wao wa maandiko ili waweze uzidisha upendo wao kwa Mungu, kwa majirani, na kwao wenyewe (Mathayo 22:37-40); Mosiah 1:49, kutetea heshima na thamani ya watu wote (Kanuni na Maagano 16:3c-d), kuifuata njia ya Yesu Kristo kwa uaminifu.

Thibitisho la Tisa

Pamoja na Wakristo wengine, tunakubali kwamba Biblia ndiyo maandiko ya msingi ya kanisa. Kwa kuongezea, Jumuia ya Kristo hutumia Kitabu cha Mormon na Kanuni na Maagano kama maandiko. Hatutumii maandiko hayo kuchukua nafasi ya ushuhuda wa Biblia au kuiboresha, bali kwa sababu vitabu hivyo vinathibitisha ujumbe wake kwamba Yesu Kristo ni Neno la Mungu Lililo Hai (Utangulizi wa Kitabu cha Mormon; Kanuni na Maagano 76:3g). Tumesikia Kristo akinena katika vitabu hivyo vitatu vya maandiko, na kushuhudia kwamba yeye "Yuko hai milele na milele" (Ufunuo 1:18).

Katika nyakati hizi zetu, tunahitaji kuishi na kufafanua ushuhuda wa maandiko kupitia kwa Roho Mtakatifu, pamoja na jumuia kwa ajili ya kazi maalum, katika jina la Mfalme wa Amani.

Picha hakimiliki Dpyancy/Adobe Stock

Maswali ya kutafakari na kujadiliwa na watu Binafsi na Makundi

1. Kwa hali ya maombi, soma thibitisho zote, maoni yako ni yapi kuhusu ulichosoma?
2. Fikiria juu ya dibaji. Unawezaje kuyafafanua maneno haya, "kufafanuliwa kwa njia ya kuwajibika", na "kutumiwa kwa njia ya uaminifu"? Mtazamo wako kuhusu maandiko unawezaje kuimarishwa ili uzingatie vigezo hivyo viwili?
3. Unasaidiwa vipi na thibitisho la Kwanza na la Pili kutofautisha kati ya neno lililo Hai (Kristo) na neno lililoandikwa (Maandiko matakatifu)? Ni vipi ambavyo mambo hayo mawili hutatanishwa katika maisha ya kanisa? Ni matatizo yapi hutokana na utata huo?
4. Ni vipi ambavyo umemtambua Kristo "katika maandiko na kupitia kwa maandiko". (Thibitisho la Pili)? Ni vipi ambavyo umepata ujumbe wa Mungu wa kuokoa na kugeuza "katika ushuhuda wa maandiko"?
5. Ni vipi ambavyo ufahamu wa mazingira ya kitamaduni na kihistoria umekusaidia kuvitumia vifungu fulani maishani mwako kwa njia ya ufafanuzi wa kuwajibika na kwa uaminifu? (Thibitisho la Tatu).
6. Ni vipi ambavyo kutambua wajibu wa waandishi wanadamu kumeathiri vile unavyotazama maandiko maishani mwako na katika maisha ya kanisa (Thibitisho la Tatu)? Ni manufaa gani


Maandiko yanatoa mwelekeo wa kutia moyo na kuelewa maisha yanapofasiriwa kwa kuwajibika na kutumiwa kwa uaminifu.



 Picha imepigwa na Jack Martin

unayo yapata katika umoja na hali tofauti ya ushuhuda wa maandiko?

7. Ni vipi ambavyo umewaona watu wakitumia maandiko kudhulumu, kuamuru, na kuwakandamiza wengine. (Thibitisho la Nne)? Unawezaje kuyatumia na kuyafahamu maandiko kwa njia bora kama mtumishi anayefuata mfano wa Yesu Kristo? Ni vipi ambavyo hali hii itakuhitaji kubadilisha vile unavyotumia maandiko?
8. Kuna uwezekano gani wa kuamini kwamba maandiko ni "Kweli" lakini hayakosi kuwa na kosa "Ni nini maana ya kuthibitisha kwamba maandiko "Yanaaminika" na yanaweza "kutegemewa vilivyo" (Thibitisho la Tano).
9. Ni vipi ambavyo wewe hutumia imani, uzoefu, desturi na utaalamu katika kusoma, kufahamu, na kuyatumia maandiko. (Thibitisho la Sita)? Ni lipi unalo sisitiza kuliko mengine? Lipi linge kunufaisha kwa kuzingatia sana?
10. Ni vipi ambavyo Roho Mtakatifu amekubariki katika ufahamu wako wa maandiko? Ni vipi ambavyo Roho Mtakatifu ali kuongoza kujua kweli mpya? (Thibitisho la Saba)? Ni vipi ambavyo maandiko yamekupa ufunuo?
11. Ni vipi ambavyo maandiko yamekusaidia zaidi "kuifuata njia ya Yesu Kristo kwa uaminifu Zaidi"? (Thibitisho la Nane) Ni vipi ambavyo imekusaidia kuzidisha upendo wako kwa "Mungu kwa jirani yako, na kwako mwenyewe"?
12. Ni vipi ambavyo unaifahamu Biblia kuwa ya msingi? Ni nini basi jukumu la vitabu vingine viwili vya maandiko (Thibitisho la Tisa).? Kwa namna gani mojawapo ya vitabu hivi vitatu vya maandiko vimetumika katika maisha na safari yako ya kiimani?



Picha hakimiliki Dopa Sorin | Dreamstime

SISI NI KITU KIMOJA, **SISI NI WENGI**

Taarifa hii ilitayarishwa wakati wa mkutano wa viongozi wa kimataifa mnamo mwaka wa 2004. Ilisomwa na kikundi kimoja katika kongamano la ulimwengu mzima la mwaka wa 2004 kama mawazo ya umoja na hali mbalimbali zinazopatikana ndani ya Jumuia ya Kristo. Taarifa hii imeendelea kutoa maoni yote ya misemo tofautitofauti ya kanisa kote ulimwenguni.

Sisi ni jumuia ya Kristo na tunasafiri pamoja katika safari hii. Tunaimba "furaha" katika maelfu ya kusanyiko zetu. Tunasema "tumaini" katika lugha nyingi. Tunatangaza amani katika mataifa yanayokaribia 60. Sisi ni kitu kimoja na sisi ni wengi. Sisi ni watu wa aina mbalimbali, ilhali sisi ni jumuia kwani sisi ni mali ya Kristo.

Tunaishi katika ulimwengu ambao uso wa Kristo umepasuliwa. Wanadamu wanaumizana na kuupasua mwili wa Kristo. Mifumo



 Picha zimepigwa na Bob Thomas

na taasisi huigandamiza roho na kuiteka akili. Kristo anaomboleza anapoona risasi, vizuizi vya magurudumu yanayochomwa, vizuizi vya kitamaduni, vurugu na sehemu zilizotapakazwa mabomu ya kutega, ziki watenganisha wanadamu. Kristo anatusaidia kubeba mzigo wa umaskini, ukimwi, mayatima, ubeberu, utajiri, ugomvi, Kristo anateseka pamoja na watu wanaoteswa kwa ajili ya jina lake na kutelekezwa watumishi wake wanapo zisahau jumuia za asili.

Kanisa pia upasua uso wa Kristo. Tunaonyesha ulimwengu mwanakondoo na simba na mtoto ilhali tunashindwa kutatua ugomvi katika familia na kusanyiko zetu wenyewe. Mara nyingi sisi huzingatia sana mahusiano yetu wenyewe kiasi cha kuwa katika hatari ya kuupoteza uhusiano wetu na Kristo ambaye upatikana pia ndani ya mgeni au adui. Sisi huwa na uhasama kwa tamaduni za mataifa mengine. Tunakumbwa na hatari ya mgawanyiko kuhusu mada zinazotia wasiwasi kama vile jinsia ya binadamu, kubatizwa tena, na kuwa mshirika. Tunang'ang'ana kuwakilisha uongozi kutoka pembe zote za ulimwengu tunapofanya uamuzi wa maswala muhimu katika maisha ya kanisa. Sisi pia tumepasua uso wa Yesu Kristo ilhali Mungu ametuchagua. Sisi ni wengi, lakini sisi ni kitu kimoja.

Jumuia

Sisi ni kitu kimoja katika jumuia. Tunatamani kuwa pamoja na kuhisi kwamba tume unganishwa na fundo lisiloweza kukatika ili kupata maskani ya kweli ndani ya kanisa.

Vile ambavyo kanisa la karne ya Kwanza lilipanuka na kujikuta katika tamaduni na vitambulisho mbalimbali, mara nyingi sisi tumeitwa kung'ang'ana na kutiwa changamoto mara kwa mara ili kupata ufahamu





Picha kutoka kwa kumbukumbu za Jumuia ya Kristo

mpya wa upendo wa Mungu ulio imara na usio na kipimo.

Tunakubali kwamba Jumuia ya Kristo ni utamaduni wa aina ya pekee. Vivyo hivyo, kila mmoja wetu ameshikilia kitambulisho cha utamaduni wetu; Kila moja ya kusanyiko zetu limeloweka katika utamaduni wa mahali ambapo kusanyiko hilo liko. Hatuja itwa ili kuacha na vitambulisho hivyo.

Pia tunajua kwamba ha tuko peke yetu katika hali ya kuwa Wakristo. Tunafanya kazi pamoja na wale wanaotangaza maadili ya Kristo. Tunajiunga na juhudi za muungano wa madhehebu yote ya Ukristo na kupambana kuwa jumuia na watu wote wa imani.

Tunahisi uchungu tunapoona washirika wa mwili wa Kristo wakiteswa, wakiwekewa mipaka, au wakidhulumiwa wanapojaribu kutoa ushuhuda wao. Tunawahurumia watu walio katika nchi zilizo na sheria zinazozuia ubatizo. Tunalia pamoja na ndugu na dada zetu ambao makanisa na nyumba na maisha yao yanakumbwa na vitisho kwa sababu ya Imani yao.

Tunang'ang'ana na maswala ya kuwa watu wa aina mbalimbali. Ni wakati gani ambao kuwa watu wa aina mbalimbali hutishia umoja wetu? Ni vipi ambavyo sisi hushughulikia maswala ambayo ni ya kutatiza katika sehemu zingine ilhali maswala hayo ni haramu katika sehemu zingine? Ni maswala yapi yanaweza kutatuliwa na nchi husika bila kuumiza ushirika wa ulimwengu mzima?

Hatuna majibu yote. Jumuia yetu ya kushirikiana inatulazimisha kutafuta majibu kwa kusikiliza mpaka tutakapoelewa. Tunaamua kusonga mbele kwa kuongozwa na upendo na huruma badala ya imani ya dini ya kulazimishwa.

Thamani ya watu

Sisi ni kitu kimoja katika kuamini kwetu kwamba kila nafsi na kila mtu ana thamani machoni pa Mungu.

Watu wote wameitwa kuendeleza vipawa vyao kwa ajili ya huduma kwa Kristo na kwa watu wengine.

Tunathamini tamaduni na lugha za watu wengine, lakini tunapigana na vizuizi vinavyotenganisha kulingana na mipaka ya hadhi, tabaka, jinsia, jamii, taifa, na umri. Tunawachukulia washirika wote wa Jumuia ya Kristo kuwa ni ndugu na dada. Mungu anayajua majina yetu. Tunasalimiana kama watu wa familia moja hata kama mtu mmoja hajajulishwa kwa mwingine.

Tuko huru kuwa na mawazo yetu wenyewe, kupambana na hali ya kuwastahili na kuwakubali watu walio tofauti nasi. Tuna husishwa. Sisi si tone katika bahari ya binadamu, sisi si sura tofauti katika kikundi cha watu. Mungu ametuita katika mahusiano ya pekee.

Ibada na Sakramenti

Sisi ni kitu kimoja katika kuamini nguvu za sakramenti na kukutana kwetu na Mungu kupitia kwa ibada.

Sisi ni wengi katika desturi zetu. Katika sehemu zingine, watu huacha

viatu nje na kuingia katika majengo ya ibada miguu mitupu. Katika sehemu zingine, sisi huvaa lofa zilizopigwa rangi na malapa ya visigino virefu. Mahali kwingine, wanawake na wanaume hawaketi pamoja kanisani, na kwingine wao huketi pamoja. Watu wengine huimba theolojia yao ilhali wengine ukariri, husoma na kuihubiri injili. Watu wengine husali kimyakimya, wengine husali wawiliwawili, na wengine husali katika sauti mbalimbali zinazoungana katika sifa na sala za dua. Sisi hukutana kwa muda wa saa moja pekee au mpaka Roho Mtakatifu aseme tumemaliza. Damu ya Kristo uashiriwa kwa maji ya zabibu, maji yatokayo ndani ya nazi, maji yaliyotiwa ndani sukari iliyounguzwa au soda ya machungwa. Mwili wa Kristo huashiriwa kwa mkate wa ngano, wa shayiri, wa mahindi, au wa mchele, lakini sote hujitwalia jina la Kristo na kumbuka, ili roho wake adumu ndani yetu.

Maandiko

Sisi ni kitu kimoja katika kuamini kwamba maandiko ni muhimu kwa uanafunzi wetu kama watu binafsi au kama kusanyiko.

Sisi ni wengi kulingana na jinsi tunavyo tumia maandiko. Wengine wetu huitumia Biblia pekee. Watu wengine wana ushuhuda ulio na nguvu kuhusu vitabu vingine kama Mormon na Kanuni na Maagano katika ibada na ushuhuda wao. Sisi utahidi tunavyoweza kutumia na kufafanua maandiko.







Picha kutoka kwa kumbukumbu za Jumuia ya Kristo



Tunatuma watu wetu duniani kote kuhudumu katika utume wa Kristo. Tunapokea watu kutoka duniani kote kama vile tungempokea Kristo.

Misheni, Amani, na Haki

Sisi ni kitu kimoja katika kujua kwamba ni lazima tufanye na wala si kuwaza pekee. Tunapenda mwelekeo unaofuatwa na kanisa letu-kushughulikia matatizo yanayowakumba wanadamu na kuunganisha amani na haki katika ulimwengu huu usiokuwa na haki. Maisha ndani ya kanisa ni halisi na utendaji, yanatoa mwelekeo katika mazingira ya sasa na vilevile kuwatayarisha watu kwa uzima baada ya kifo.

Tuna njia nyingi za kuwaendea watu. Sisi huenda katika magereza, hospitali, kwa wenye njaa, kwa wasiokuwa na makao. Sisi hujitahidi kuubadilisha ulimwengu, sisi uthubutu; kuzungumza juu ya mambo yaliyo



magumu kujadiliwa. Sisi huwaendea watu ambao ni wagumu kufikiwa. Sisi huenda katika sehemu hizo kujenga "Sayuni", kujenga jumuia. Sisi huwaendea wananchi wa asili, wahamiaji, wakurugenzi wa benki, walevi, watu wa hadhi ya chini, watu wa hadhi ya juu. Sisi huwaendea watetezi wa serikali, wahakiki wa jamii na siasa. Sisi huwatuma watu wetu ulimwenguni kote ili waweze kuhudumu katika misheni ya Kikristo. Sisi huwapokea watu kutoka ulimwengu wote vile ambavyo tungepokea Kristo.

Kushirikiana

Sisi ni kitu kimoja katika ukarimu. Tuna njia nyingi za kutoa. Sisi hucheza kwa furaha tunapotoa sadaka na pia huketi kimya sahani inapo pitishwa kanisani. Sisi hutoa fungu la kumi kama tunavyo ongozwa na Roho wa Mungu na kwa kutuma pesa kwa benki kila mwezi. Sisi hutoa malimbuko na pia hutoa pesa zilizobaki. Sisi hutoa lulu nyeusi na pia hutoa kuku walio hai.

Sisi ni kitu kimoja tumeitwa kuwaeleza wengine kuhusu injili.

Sisi ni wengi katika mitindo wetu. Sisi huhubiri barabarani; huweka hema katika mitaa ya vijiji vyetu. Sisi huenda kuhubiri nyumba kwa nyumba, hutumia vipaza sauti. Sisi hushiriki tukiwa faraghani, hutangaza katika redio, huimba katika kwaya, na humshawishi chifu ili tuweze kuliingiza kabila fulani katika Imani. Sisi hutoa majadiliano ya kuridhisha, na pia huepuka mijadala kwani huwa tunahofu kwamba kwa kuishinda mijadala hiyo huenda tuka wakosa rafiki zetu. Tunafunza kwamba"Kila Mmoja, Amfikiye kwa Mmoja" tunafunza kwamba " Kila Mmoja, Amfikiye Mtu Mmoja kila mwezi".

Imani katika Yesu Kristo

Sisi ni kitu kimoja, sisi ni wengi. Sisi huimba kwa njia tofauti, huomba kwa tofauti, huhubiri na kuishi na kuyatazama mambo na kuwaza kwa njia tofauti.

Hata hivyo, sisi ni kitu kimoja! Yesu, ambaye ni Kristo. Yeye ni umoja wetu. Tuna imani ndani yake. Yeye ametufanya kuwa kitu kimoja.

Sisi humwimba yeye, humwomba yeye, humhubiri, humwona, na kumwaza yeye.

Yeye ni Yesu wa historia, mwanadamu kamili. Mungu kamili. Mfano wake ni muhimu kwetu. Alisulubiwa, akafa, akazikwa, akafufuka. Aliishi na anaishi kwa ajili yetu na ndani yetu.

Mwokozi. Mwokozi wangu, Mwokozi wako, Mwokozi wetu. Mwokozi wa wapotevu; watu binafsi wapotevu. Vijiji vipotevu, watu wote wapotevu. Tulikuwa tumepotea, lakini sasa tume patikana. Hatukuwa tumependwa. Sasa tunapendwa.

Sisi ni kitu kimoja. Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu.

Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Utatu.

Utatu katika mmoja umeunganishwa. Umoja. Jumuia .

Sisi ni kitu kimoja.

Yeye hutuhukumu, hutusamehe, anatupenda, anatulilia, na analia nasi. Anarudi tena. Yuko nasi.

Si wengi wetu. Si mmoja wetu. Sisi sote. Sisi ni kitu kimoja. Alituita. Amekuita. Anakuita. Pamoja.

Tunaiinua jina: Yesu Kristo. Tunamshuhudia Yesu Kristo. Sisi na yeye. Sisi ni kitu kimoja.



 Picha imepigwa na Wayne Rowe

TAFAKARI ZAIDI

• Uzoefu wako ni upi na unafahamu nini kuhusu kanisa kote ulimwenguni?

• Ni kitu gani kinacho kushangaza katika kauli hii?

• Taarifa hii inatueleza nini kuhusu utambuzi na misheni?

• Maoni yako ni yapi kuhusu wazo hili linalosema kwamba tumekita mizizi ndani ya desturi zetu wenyewe na vilevile sehemu ya desturi ya Jumuia ya Kristo?

• Desturi hizo zinaingiliana vipi katika mazingira yako?

• Kauli hii inauliza maswali yafuatayo: Ni wakati gani ambapo kuwa watu wa aina mbalimbali huwa tishio kwa umoja wetu? Ni maswala gani yanaweza kufanyiwa uamuzi mashinani bila kuudhuru ushirika wetu wa ulimwengu mzima? Fikiria jinsi ungejibu maswali hayo nje ya asili ya kanisa lako.



Sio wengi wetu.
Sio mmoja wetu.
Sisi sote.
Sisi ni kitu kimoja.
Alituita.
Anatuita.
Amekuita.
Anakuita.
Pamoja.



MITAZAMO KUHUSU HISTORIA YA KANISA

Msingi na chanzo endelevu cha imani yetu ni ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo.

Historia nzuri hufahamisha imani, na imani yenye afya inaongoza kwenye maarifa kuhusu historia.

Na Raisi
Stephen M. Veazey
October 1, 2008

Nyundo ya mwenyekiti iliyotumiwa na Joseph Smith wa Tatu alipoongoza kongamano za kanisa iko juu ya meza ndogo ndani ya ofisi yangu iliyo katika jengo la Hekalu. Nyundo hii si yangu; ni ya kanisa.

Mara chache ninapowaza juu ya masuala magumu ya kanisa, mimi huiinua nyundo hiyo na kutazama kwa heshima kichwa chake cha pembe kilichopasuka kidogo na mkono wake wa mbao uliotengenezwa vizuri sana. Ninaposhika mkononi mwangu, mimi huhisi kwamba nina uhusiano halisi na siku za zamani. Mimi hufikiria juu ya watu, matukio, na hali zilizounda kanisa la sasa.

Ingawa nimesoma vitabu vya historia ya kanisa, mimi hutaka kujua mengi kuhusu babu zangu wa kidini na mazingira ya kihistoria waliyokuwa ndani walipo dhihirisha imani yao.



Kazi ya msanii wa Nauvoo, Illinois, iliyokuwa makao makuu ya zamani ya kanisa.

Hapo awali niliijua historia ya kanisa kwa hali ya kawaida tu, lakini tangu nilipo teuliwa kuwa raisi wa kanisa, nimejitahidi kusoma kwa mapana na marefu hadithi yetu. Nimechunguza vitabu na Makala mengi ya wasomi, waandishi, wachapishaji, wanaoamini na wanaoshuku na walio katikati. Ukweli hauogopi kuchunguzwa.

Katika kipindi cha miongo ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la habari kwani wanahistoria wa kidini wameweza kupata vitabu vingi vya marejeo na wameweza kuandika na kusema wazi kuhusu mada mbalimbali. Vilevile, katika miaka michache iliyopita, mwangaza wa vyombo vya habari pamoja na mfululizo wa hali ya juu wa stesheni mbalimbali za televisheni na kampeni za kisiasa-zimekuwa zikizungumzia historia ya watakatifu wa siku hizi.

Kutokana na uchunguzi wangu wa maandishi mbalimbali ya kuaminika, mazungumzo kati yangu na wanahistoria kutaka kuchunguza mambo kwa undani, baadhi ya mawazo niliyokuwa nayo hapo awali yamepata changamoto na kurekebishwa katika mazingira ya ufahamu uliongezeka. Mtazamo wa "utetezi" kuhusu historia ya kanisa-kuwasilisha historia yetu kwa hali ya kupendeza mno hakutoshelezi safari iliyo mbele yetu. Mtazamo huo hauonyeshi ukamilifu unaostahili kuwa muhimu kwa ushuhuda na huduma yetu.

Ingawa nimerekebisha baadhi ya mitazamo yangu binafsi, kwa kiasi kikubwa nimeweza kupata ufahamu mpana wa hali husika zilizo ngumu kuelezeka zilizounda kanisa kwa miaka mingi iliyopita. Nimeweza kuona wazi kabisa vile Roho wa Mungu alifanya kazi ndani ya maisha ya watu waliokuwa na upungufu,

lakini walikuwa wamejitoa kikamilifu na akawatumia kuunda mwendo wa imani unaoendelea kutekeleza sehemu muhimu katika makusudi ya Mungu yanayojitokeza wakati wa sasa. Kutokana na hayo, nina matumaini makubwa zaidi kwamba yule Roho aliye wezesha kanisa kupitia changamoto zisizoweza kushindika nyakati hizo za zamani, atazidi kutuendeleza na kutuongoza katika siku za usoni.

Uraisi wa kwanza umejiunga na watu wengine kuchunguza masuala yanayoibuka kutokana na uchunguzi unaoendelea wa historia ya urudishaji, tuliamua kwamba wakati umefika wa kuwasilisha kundi la "Kanuni za Historia ya Kanisa" zitakazosaidia kuongoza mawazo na mazungumzo ya kanisa. Kanuni hizi zimetiririka kutoka kwa utambuzi wa viongozi wa kanisa la ulimwengu mzima, wanahistoria wa kanisa , wanateolojia na watu wengine wa zamani na walioko sasa. Tunatumaini kwamba kauli hizo zitaweza kutoa usaidizi kanisa linapoendelea kufanya uchunguzi juu ya watu, matukio, na maana ya hadithi ya kuvutia ya kanisa.

Kanuni za Historia ya Kanisa

1. Kuendelea kuichunguza historia yetu, ni sehemu ya uundaji wa kitambulisho.

Sisi kama kanisa hutaka kila mara kueleza wazi kitambulisho, ujumbe , na misheni yetu. Katika hadithi yetu ya imani, tunaona waziwazi Roho




Joseph Smith wa Tatu,
Rais wa kanisa kutoka 1860-1914

wa Mungu akipa jumuia hii ya Imani vifaa, ufunuo, na uzoefu kwa ajili ya makusudi ya kiungu. Watu walio na kumbukumbu ya pamoja ya siku zao za zamani, pamoja na ufahamu wa kuambiwa maana yake, wame jitayarisha vilivyo kuelekea katika siku za baadaye.

2. Historia hutupasha habari lakini haiamrishi imani yetu au mambo ya msingi ya imani yetu.

Msingi na asili ya imani yetu ni ufunuo wa Mungu ndani ya Yesu Kristo. Kuichunguza historia hakuhusu kuthibitisha au kukanusha matukio ya miujiza, ya kiroho, au ya ufunuo yanayoanzisha au kugeuza mwendo wa kidini. Historia ya busara huiarifu Imani, na imani nzuri u wapa watu ujuzi kuhusu historia. Theolojia na Imani, ikiongozwa na Roho Mtakatifu, inatakiwa kuchukua



Kutawazwa kwa rais Veazey mwaka 2005

sehemu muhimu ya kutambua maana ya kudumu ya matukio kama hayo pamoja na ukweli unaopatikana katika matukio hayo. Ufahamu wetu wa historia yetu huathiri Imani yetu na mambo ya msingi ya imani. Hata hivyo, maisha yetu ya awali haifanyi imani yetu na mambo ya msingi ya imani yetu kubaki vile yalivyokuwa kihistoria.

3. Kanisa linahimiza utaalam wa kihistoria ulio wa kweli na wa kuwajibika.

Kujifunza historia huhusisha Nyanja zingine za kitaaluma zinazohusiana na historia hiyo. Wanahistoria hutumia utafiti wa kitaaluma ili kupata ukweli mwingi iwezekanavyo; kisha wao hufafanua ukweli huo ili kutunga maelezo yaliyo wazi kabisa kuhusu mambo yaliyokuwa yakitendeka nyakati za zamani. Vile vile wao huchunguza utamaduni wa binadamu ili waweze kuona vile uliathiri matukio mbalimbali. Wanahistoria hujaribu kuelewa mikondo ya maana ili waweze kufafanua ni maana gani ambayo nyakati za zamani zinaleta katika siku zetu za usoni. Njia hii inatakiwa kuepuka kufafanua nyakati za zamani kulingana na mtazamo wa sasa kuhusu ulimwengu na utamaduni badala ya kufafanua utamaduni wa nyakati husika.

4. Uchunguzi wa historia ya kanisa ni safari inayoendelea.

Tukisema kwamba kitabu kimoja cha historia ndicho kinachosema hadithi ya kweli, tutakuwa tunaingia katika hatari ya kuifanya aina moja ya masimulizi kuwa "takatifu", jambo lililoonekana katika nyakati za zamani. Jambo hilo huzuia kupata ujuzi Zaidi kutokana na uchunguzi unaoendelea. Uchunguzi nzuri wa kihistoria ufahamu kwamba uamuzi unaweza kurekebishwa mara tu ufahamu na habari mpya inapopatikana kutokana na uchunguzi unaoendelea.

5. Kuuona uaminifu pamoja na upungufu wa kibinadamu katika historia yetu kunahifanya iwe ya kuaminika nay a kweli.

Historia yetu ina hadithi nyingi za imani kuu na ujasiri zinazotutia moyo. Vilevile hadithi yetu ina viongozi waliosema na kufanya mambo yanayoweza kutushtua kulingana na mtazamo wetu wa sasa na utamaduni wa sasa. Wanahistoria hujaribu

sana kukosa kuhukumu, badala yake wao hujaribu kuelewa mambo kwa kujifunza mambo mengi iwezekanavyo kuhusu muktadha na maana ya maneno na matendo ya nyakati hizo. Matokeo yake huwa ni uwezo wa kuhisi maono ya mwingine badala ya kumuhukumu.

Maandiko yetu yana msimamo wa kuonyesha kwamba Mungu, kwa neema yake huwatumia watu walio na upungufu ili kutekeleza huduma na uongozi unaohitajika.

6. Uchunguzi wa kuwajibika wa historia ya kanisa unahusisha kujifunza, toba, na mgeuzo.

Kanisa lenye misheni inayozingatia ukuzaji wa jumuia za furaha, tumaini, upendo na amani linatakiwa kusema kweli kuhusu historia yake. Ni muhimu kwetu kukiri ni wakati gani tumekosa kuwa vile injili ya Yesu Kristo inatuhitaji tuwe. Uaminifu huu utushawishi kutubu, na pia utaimarisha msimamo wetu. Kukubali makosa yaliyofanyika hapo awali utusaidia kuepuka kurudia makosa hayo na utuweka huru kutokana na ushawishi wa udhalimu na vurugu ya nyakati za zamani katika historia yetu. Ni lazima tuwe wanyenyekevu na tuwe tayari kutubu, kila mtu binafsi na pia kama jumuia, ili tuweze kuchangia katika kuirudisha Shalomu ya Mungu hapa duniani.

7. Kanisa linadesturi ya zamani sana ya kuwa halitungi sheria wala kutoa maagizo kuhusu mambo ya historia ya kanisa.



Wanahistoria wanatakiwa kuwa huru kutoka maoni yao badala ya kuzingatia ushahidi vilivyo. Kwa kuchunguza kwa makini na kuongozwa na Roho Mtakatifu, kanisa linajifunza namna ya kukubali na kuifafanua historia yake yote kwa njia ya kuwajibika. Hii ni pamoja na kuiweka habari mpya na ufahamu unaobadilika katika mtazamo unaostahili na vilevile kuusisitiza sehemu za historia yetu zinazoendelea kuchukua nafasi muhimu katika kuelekeza kitambulisho na misheni ya kanisa wakati wa sasa.

8. Tunatakiwa kuunda desturi ya kuheshimika ya kuwa na majadiliano juu ya masuala ya historia.

Tusiweke hadithi yetu ya imani mipaka ya mtazamo mmoja pekee.



Nyumba ya familia ya Smith huko. Nauvoo, Illinois.

Mitazamo mbalimbali hutupa ufahamu mkubwa wa matendo ya Mungu katika hadithi yetu takatifu. Bila shaka, wanahistoria watakuwa na maoni tofautitofauti wanapofanya uchunguzi. Kwa hivyo ni muhimu kwetu kuunda na kuunga mkono desturi ya kuheshimika inayokubali mitazamo tofautitofauti kuhusu historia. Mazungumzo yetu kuhusu historia yanatakiwa kuwa ya upole na yenye lengo la kujaribu kuielewa mitazamo ya wengine. La muhimu zaidi, tunatakiwa kuendelea kuzingatia mambo yaliyo muhimu Zaidi kuhusu ujumbe na misheni ya kanisa katika nyakati hizi.

9. Imani yetu imejengwa katika msingi wa ufunuo wa Mungu ndani ya Yesu Kristo na katika uongozi unaoendelea wa Roho Mtakatifu.

Mioyo yetu na akili zetu vinatakiwa kuendelea kuzingatia ufunuo wa Mungu ndani ya Yesu Kristo. Kama neno la Mungu lililo hai katika historia ya binadamu, Yesu Kristo alikuwa na hata sasa yeye ni msingi wa imani yetu na zingatio la misheni na ujumbe wa kanisa.

MUHTASARI

Ni matumaini yetu kwamba umeweza kuhisi Roho wa Mungu akitembea na kukugusa ulipokuwa ukisoma waraka huu wa kushirikiana katika Jumuia ya Kristo: Kuchunguza kitambulisho, misheni, ujumbe, na imani. Rudia kusoma waraka huu mara kwa mara kwa njia ya maombi.

Yatafakari maswali yanayokupa changamoto. Jiunganishe tena na misemo hii ya misheni, ujumbe na imani yetu inayokuwa. Endelea kujiachilia kwa kazi ya Roho wa Mungu ndani ya maisha na huduma yako.





Picha imepigwa na David Wheaton